**HATIMA** kesi ya kina Mdee Desemba 14



UKURASA 2

**RAIS** Dk. Mwinyi acharuka ujenzi holela Zanzibar



UKURASA 4

**HOSPITALI** yapima haja kubwa kugundua TB

UKURASA 4


# Nipashe

Jumatano Oktoba 25, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581474

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## WATKINS AITAKA EURO 2024

UKURASA 22

## Waziri aagiza UDART itafutiwe washindani

UKURASA 3

### KESI MAUAJI ANETH MSUYA

# Mke wa Bilionea Msuya akana alichokiri Polisi

UKURASA 7



Mshtakiwa Miriam Mrita, akiteta jambo na Wakili Peter Kibatala katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana, kabla hajaanza kusikiliza kesi inayomkabili ya mauaji ya wifi yake, Aneth Msuya. **PICHA: IMANI NATHANIEL**



Rais Samia Suluhu Hassan akiweka shada la maua kwenye kaburi la Rais wa Kwanza wa Zambia, Hayati Kenneth Kaunda, jijini Lusaka jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA 2

# Samia: Zambia karibuni, mna bandari kavu hekta 20 kwetu

UKURASA WA 22

## MODRIC HAONDOKI REAL MADRID

MKURUGENZI wa Real Madrid, Jose Angel Sanchez, amekanusha ripoti kwamba Luka Modric anaweza kuondoka kuelekea Saudi Arabia Januari. Modric amekiri wazi...

UKURASA WA 24

## GAMONDI: YANGA INACHEZA KIBINGWA



BAADA ya kukiongoza kikosi chake kuibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Azam FC juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema...

**MICHEZO** AZIZ KI KINARA MABAO YA FAULO LIGI KUU BARA UK. 23

**KATUNI** UK. 6

# Samia: Zambia karibuni, mna bandari kavu hekta 20 kwetu

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema Tanzania na Zambia zitaendelea kuweka mazingira rafiki ya usafirishaji huru wa bidhaa na watu ili kuimarisha uhusiano wa kibiashara na kuwainua kiuchumi wananchi wa nchi hizo.

Aliyasema hayo jana katika Maadhimisho ya Miaka 59 ya Uhuru wa Zambia yaliyofanyika katika Viwanja vya Ikulu ya nchi hiyo na kuongeza kuwa mikakati ya ushirikiano wao inalenga kutimiza haja za wananchi.

Rais Samia alisema katika kuboresha ushirikiano wa kibiashara kati ya nchi hizo, Tanzania imetenga hekta 20 za ardhi kwenye Bandari Kavu ya Kwala iliyoko ili kupatia nchi hiyo nafasi kubwa ya kuhifadhi makasha yanayotoka Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema hatua hiyo itapunguza msongamano na ucheleweshaji mizigo ya Zambia na kupunguza gharama za kufanya biashara kati ya nchi hizo.

"Tunapozungumzia mgawanyo sawa wa rasilimali, tunasisitiza haja ya watu kuwa katikati ya mipango yetu. Kwa Wazambia na Watanzania ambao wanatusikiliza leo (jana), ninataka kukuhakikishia kuwa Rais (Hakainde Hichilema) na mimi ni waumini wa maendeleo ya uchumi wa watu," alisema.

Rais Samia alisema dhamira ya Tanzania ni kuimarisha ushirikiano, ufungamano na urafiki kati ya mataifa hayo ili kufikia malengo, dira na ustawi wa nchi zao.

Aliipongeza nchi hiyo kwa kusherehekea miaka 59 ya uhuru na kuwakumbusha kuitumia siku hiyo kutafakari na kuthamini mchango wa waliowatangulia wa kujitoa mhanga ili nchi hiyo ipate uhuru kama taifa moja.

Rais wa Zambia, Hichilema, aliishukuru Serikali ya Tanzania na watu wake kwa kumruhusu Rais Samia kutumia siku tatu nchini humo na kuhudhuria shughuli hiyo muhimu licha ya kuwa na mambo mengi ya kufanya katika nchi yake.

Alimshukuru Rais Samia kwa kuja na kundi la wafanyabiashara katika nchi hiyo kwa ajili ya kutangaza fursa za kiuwekezaji hali itakayochangia kutoa ajira kwa wananchi kukuza uchumi wa nchi hizo.

Alisema nchi hizo kijiografia zimeunganishwa kupitia mipaka ambayo inawaweka pamoja watu wa mataifa hayo kibiashara, uhusiano, ndoa na kuzisihi serikali zake kutumia fursa hizo kuwanufaisha wananchi wao kiuchumi kupitia uwekezaji.

Rais huyo alisema serikali za nchi hizo zina kazi kubwa ya kuendeleza kazi zilioachwa na waasisi wake Hayati Julius Nyerere na Kenneth Kaunda kama vile kukarabati reli ya TAZARA inayounganisha nchi hizo, ili kufungua fursa zaidi za kibiashara, kupanua mabomba ya gesi.

"Jana (juzi) usiku nilisema tukiwa kama sehemu ya SADC (Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika) na Afrika, tuna jukumu lisiloepukika kuimarisha uhusiano wetu, ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya barabara, mawasiliano, teknolojia nyingi za kidijitali na chakula," alisema.

Rais Hichilema pia aliwataka viongozi wakuu wa nchi za SADC, Afrika na dunia kwa ujumla kuimarisha amani katika nchi zao ili ziendelee kuwa na uchumi imara.



Alitolea mfano namna vita vya Ukraine na Urusi vilivyoyumbisha uchumi wa nchi nyingi duniani zikiwamo Tanzania na Zambia.

"Tunataka kutoa wito kwa kila kiongozi duniani, kuwa na matendo ambayo yatadumisha amani, usalama na utulivu katika nchi zao, kanda, bara na dunia ili kuzingatia uwekezaji wa biashara, uchumi, maendeleo ya kijamii," alisema.

## Daktari Bingwa ataja makundi yaliyo hatarini vidonda vya tumbo

**Na Christina Mwakangale**

WANAOKAA muda mrefu bila kupata mlo, wametajwa ni miongoni mwa waliomo katika hatari ya kupata vidonda vya tumbo.

Vilevile, wenye msongo wa mawazo, wamo katika hatari hiyo huku ulaji wa vyakula vyenye kiwango kikubwa cha 'acid' kama vile maziwa ukitajwa kuwa miongoni mwa vyanzo vya maradhi hayo.

Bingwa wa Upasuaji na Mkuu wa Idara ya Upasuji Hospitali ya Taifa Muhimbili – Mloganzila, Dk. Eric Muhumba, alibainisha hayo jana katika mazungumzo na mwandishi aliyetaka kufahamu ugonjwa huo ambao umekuwa tishio katika jamii.

"Kwa siku, kati ya wawili hadi watano wanafika hapa hospitalini wakibainika kuwa na vidonda vya tumbo. Wengi ni watu wazima," alisema bingwa huyo.

Alifafanua: "Stress (msongo) za maisha, kukaa na njaa kwa muda mrefu, kula vyakula vya jamii ya maharage, vyakula vyenye viungo vingi, maziwa ni miongoni mwa vyanzo vya vidonda vya tumbo," alisema Dk. Muhumbwa.

Alisema kuna athari kubwa ya vidonda vya tumbo kama vile kuta za tumbo kuvimba na kuziba njia ya chakula kuingia kwenye utumbo mdogo, jambo ambalo linaweza kuhitaji upasuaji.

***USIKOSE MAKALA MAALUM KUHUSU UGONJWA HUU KATIKA TOLEO LETU LA ALHAMISI**

# Hatima ya kesi kina Mdee Desemba 14

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masijala Kuu inatarajia kutoa uamuzi Desemba 14, mwaka huu, katika shauri la Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee na wenzake 18 wanaopinga kufukuzwa uanachama Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Mahakama imefikia uamuzi huo jana baada ya kujiridhisha kwamba pande zote zimeshawasilisha majumuisho ya mwisho ya shauri hilo.

Jaji Cyprian Mkeha awali alielekeza pande zote zipewe nakala za mwenendo wa kesi hiyo Septemba 21, mwaka huu na ziwasilishe mahakamani majumuisho ya hoja zao Oktoba 19.

Mahakama ilipanga shauri hilo kutajwa jana kuangalia kama pande zote zimekamilisha kuwasilisha hoja na kisha kupanga tarehe ya uamuzi.

Wabunge 19 wa viti maalumu waliofukuzwa uanachama CHADEMA, walifunga usikilizwaji wa kesi yao Septemba 7, mwaka huu, baada ya kuwahoji wajumbe sita kati ya saba wa Bodi ya Wadhamini wa chama hicho.

Mawakili wa kina Mdee ni Ipilinga Panya (kiongozi wa jopo), Edson Kilatu na Aliko Mwamanenge, ambao katika sehemu ya maswali kwa mjumbe Francis Mushi, walihoji kuhusu taratibu zilizotumika kuwavua uanachama kina Mdee na mchakato wa uteuzi wao.

Katika majibu yake Mushi alidai anayemtangaza mtu kuwa mbunge ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na kwamba hakuna mtu anayeweza kwenda kuapishwa bila kutangazwa na Tume.

Alidai, hakuwa mjumbe wa Kamati Kuu iliyowavua uanachama kina Mdee wala mjumbe wa Baraza Kuu lililotupilia rufani ya kina Mdee, na kwamba hakujua yaliyojiri katika kikao.

Katika kesi hiyo kina Mdee wanapinga uamuzi wa Baraza Kuu la CHADEMA kutupilia mbali rufani zao za kupinga uamuzi wa Kamati Kuu kuwafukuza uanachama kwa tuhuma za kuapishwa kuwa wabunge bila ridhaa ya chama.

Kamati Kuu iliwavua uanachama wa chama hicho Novemba 27, 2020. Walikata rufani Baraza Kuu kupinga uamuzi huo wa Kamati Kuu, lakini Baraza Kuu katika uamuzi wake wa Mei 11, 2022, ulitupilia mbali rufani yao.

Baada ya uamuzi huo, wabunge hao wakakimbilia mahakamani ambako kwanza waliomba na wakapata kibali kufungua shauri hilo.

Wanapinga uamuzi wa Baraza Kuu pamoja na mambo mengine wakidai kuwa hawakupewa haki ya kusikilizwa, ambayo ni ya msingi.

Wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi huo, iamuru CHADEMA kutimiza wajibu wake kisheria, yaani kuwapa haki ya kuwasikiliza na itoe zuio kwa Spika na NEC kuchukua hatua yoyote mpaka malalamiko yao yatakapoamuriwa.

Mbali na CHADEMA kupitia Bodi ya Wadhamini, wadaiwa wengine ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye anasimama kwa niaba ya Bunge la Tanzania; na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec).

Awali, jopo la mawakili wa CHADEMA likiongozwa na Peter Kibatala, liliwaita kwa amri ya mahakama wabunge wanane kati ya 19 wafike kizimbani, akiwamo Mdee kwa ajili ya kuwahoji kuhusu na malalamiko yao waliyoyaweka katika kiapo chao walichokiwasilisha mahakamani ambao ni ushahidi wao.

Wengine walioitwa walikuwa ni Nusrati Hanje, Ester Matiko, Ester Bulaya, Grace Tendega, Jesca Kishoa, Cecilia Pareso na Hawa Mwaifunga.

Hata hivyo, mawakili wa CHADEMA waliamua kufunga mahojiano bila kuwahoji Mdee, Bulaya na Matiko, licha ya kuwaita.

Waliohojiwa ni Dk. Azavery Lwaitama, Silvester Masinde, Ruth Mollel, Ahmed Rashid Hamis, Maulida Anna Komu na Francis Joseph Mushi, ambaye alikuwa wa mwisho kuhojiwa.


Form 106a

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

**Notice of appointment of receiver or manager**
**Pursuant to Section 106(1) of the Companies Act 2002**

To the Registrar of Companies

Company Number: 69682

Name of company (Full Name): PRINCE AFRICA LIMITED

We **I&M BANK (T) LIMITED** of P.O. Box 1509, Dar es Salaam, Tanzania give notice that **ANNETTE WANGECI KIRETHI** of **HALLMARK ATTORNEYS (name of the Firm/Office) P.O. BOX 13811 DAR ES SALAAM,** Tanzania was appointed as Receiver Manager of the property of the Company with the mandate provided under the Deed of Appointment and the law.

The appointment was made by **I&M BANK (T) LTD** under the powers contained in the **DEBENTURE DEED DATED 24th September 2010 and First Deed of Variation of Debenture dated 16th August 2012 and Second Deed of Variation of Debenture 8th May 2014 and Third Deed of Variation of Debenture dated 3rd April 2017** which created a charge over all fixed and floating assets of the Company together with the current assets of the Company, both present and future including goodwill assets books and properties within the charges in the name of **I&M BANK (T) LIMITED** (a copy of the Deed of Appointment is annexed).

Name: Krishnan Ramachandran Signature: ...

Designation: Head of Corporate Banking Date: 19/10/2023

[SEAL]

Name: Veronica Magongo Signature: ...

Designation: Head of Finance Date: 19/10/2023

88/128

FOR OFFICIAL USE ONLY.

217666802

# ‘UDART itafutiwe washindani’

● Magari binafsi yalipie kupita mwendokasi

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, ameuagiza Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) kutafuta watoa huduma wengine wa njia za mabasi hayo ili kuleta ushindani na kuondoa malalamiko ya abiria kurundikana vituoni.

Pia amewataka watumishi wa DART kuwa wabunifu na waache kufanya kazi kwa mazoea kwa kuwa kuanzia sasa atakaposikia malalamiko ya kuchelewa kwa mabasi vituoni, wahusika wote watawajibika kwa uzembe huo. Aliagiza hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na menejimenti ya DART kabla ya ziara yake ya kukagua njia za mabasi yaendayo haraka (BRT).

“Mtendaji Mkuu wa DART, mimi utendaji wa mazoea kwangu haupo na mkitaka kujua ulizeni nilikotoka wananijua vizuri. Sitaki kuwapa Watanzania msongo wa mawazo, nikisikia watu wanalalamika mabasi yamechelewa vituoni, hawajui mabasi yatakuja saa ngapi, taarifa hakuna, nitakuja nitafukuza kazi watu waliohusika na uzembe huo. Mimi huwa sina mchezo mchezo,” alionya.

“Ninarudia tena, boresheni huduma za mabasi. Hili kwangu halina mjadala na bahati nzuri mimi ni mtu wa kuchukua hatua, sitosita kumchukulia hatua mtu atakayezembea, kuanzia leo (jana) hii nikitoka ofisini kwenu sitaki kusikia malalamiko yoyote, fanyeni kazi muwe wabunifu zaidi mkifahamu fika kwamba wazembe wote nitawaondoa,” alionya.

Waziri huyo alisema inashangaza kuona Tanzania ikiwa na mipango mingi ambayo imesababisha baadhi ya mataifa kuja kuichukua na kwenda kuitekeleza kwenye mataifa yao na kuleta matokeo mazuri wakati kwa upande wa Tanzania mipango hiyo inaendelea kukaa makabatini.

“Watu wanalalamikia mrundikano wa abiria vituoni, mabasi hayafuati ratiba. Sasa mjipange muwe na mabasi yanayotosheleza ruti zote. Watu wananunua tiketi, wanataka kusafiri wakute mabasi wapande waende kazini na wanapotoka kazini kwenda nyumbani wakute mabasi,” alisema.

Aliitaka DART kusimamia mtoa huduma UDART kuhakikisha mabasi yote yaliyoharibika yanatengenezwa na kuingizwa barabarani kuwahudumia Watanzania ili kuondoa malalamiko ya abiria kurundikana vituoni.

“Ninawaagiza tafuteni mtoa huduma zaidi ya mmoja wa mabasi yaendayo haraka na hatua hii itasaidia ushindani kwenye huduma hii. Hatutaki mtoa huduma mwenye maringo na ambaye hana mtaji wa kutosha, hizi njia zote tafuteni mtoa huduma zaidi ya mmoja ili kuboresha huduma kwa sababu kutakuwa na ushindani,” aliagiza.

Aliwataka DART kufuatilia mifumo yote ya kielektroniki kuhakikisha inafanya kazi ili kufuatilia mwenendo wa mabasi kufika vituoni kwa wakati kwa kuwa baaadhi ya mabasi yamekuwa yanalalamikiwa kutofuata ratiba na kusababisha msongamano. Kuhusu matumizi mabaya ya njia za mabasi yaendayo haraka, Mchengerwa alisema serikali imetumia fedha nyingi kujenga barabara hizo kwa mkopo wa Benki ya Dunia (WB), hivyo DART iangalie uwezekano wa watu kulipia kwa ajili ya kupita kwenye njia hizo ili kurejesha mkopo huo mapema.

“Fikirieni kibiashara kwa sababu huu ni mkopo wa WB ambao tutalazimika kuurejesha. Kwa hiyo, lazima tuwe na mkakati wa kukusanya fedha nyingi tukarejesha mkopo huu mapema zaidi ila kwa sasa elimisheni watu wasiohusika wasitumie njia hizo kwani ni hatari kwa mabasi ya mwendo wa haraka,” aliagiza.

Alimtaka mtoa huduma wa njia za mwendokasi, UDART, kusimamia nidhamu ya madereva kabla hawajaajiriwa kwa kuwa wengi wamekuwa wanasababisha ajali za kizembe na wakati mwingine kutongana wenyewe kwa wenyewe.

Kuhusu karakana iliyojengwa eneo la Jangwani, Mchengerwa alisema eneo hilo halifai kutokana na mafuriko yanayotokea wakati wa mvua, hivyo kuwashauri kuongeza kasi ya kutafuta maeneo mengine ya kuhamishia karakana hiyo.

# Dereva lori ashikiliwa madai kusababisha ajali, vifo 18

**Na Benny Kingson,** TABORA

JESHI la Polisi mkoani Tabora linamshikilia dereva wa lori la mafuta, Tallick Laufi, kwa madai ya kusababisha vifo vya watu 18 na kujeruhi 35 akiwamo dereva wa basi Dickson Rahimu, aliyevunjika viungo na kukazwa hospitali.

Kamanda wa Polisi mkoani Tabora, ACP Richard Abwao, alisema dereva wa lori alimsababishia kuvunjika viungo dereva wa basi katika tukio lililotokea Oktoba 21, maeneo ya Usongo, wilayani Nzega.

Ajali hiyo ilihusisha lori hilo lenye namba za usajili T 481 AGB ambalo lilikuwa likitokea jijini Dar es Salaam kwenda Mwanza na ilielezwa kuwa dereva wa lori alikuwa katika mwendo kasi akitaka kuyapita magari mengine ndipo alipoligonga basi hilo lenye namba T612 CQD lililokuwa likitolea jijini Mwanza kuelekea Dar es Salaam.

“Ajali hii imesababisha vifo vya watu 18 na kujeruhi 35 na kati yao 19 walipelekwa Hospitali ya Nkinga akiwamo dereva wa basi na wengine waliruhusiwa baada ya kupata matibabu, 15 bado wanaendelea kutibiwa,” alisema.

Abwao alisema, majeruhi wengine 31 walipelekwa Hospitali ya Wilaya Nzega, kati yao 26 waliruhusiwa na watano wanaendelea na matibabu, mmoja amepelekwa Hospitali ya Rufani Bugando Mwanza kwa uchunguzi zaidi.

Aliwataka madereva wa magari na wanaotumia vyombo vya moto kuchukua tahadhari wawapo barabarani na kuzingatia sheria zote husika ili kuepukana na ajali zinazopoteza maisha ya watu na mali zao na kuwasbabisha ulemavu wa maisha.

Uchunguzi wa gazeti ili imebaini kuwa basi hilo lilikuwa limepakia abiria zaidi ya 70 kupita kiwango kinachotakiwa kisheria.




**NOTICE OF APPOINTMENT OF A RECEIVER AND INVITATION FOR BIDS FOR SALE OF PLANTS AND MACHINERY LOCATED AT PLOT NO. 129 & 130 BLOCK 216 KIPAWA INDUSTRIAL AREA, ILALA DAR ES SALAAM**

1. **Notice**
Notice is **HEREBY GIVEN THAT** under power contained in the Debenture Deed dated 24th September 2010 and First Deed of Variation of Debenture dated 16th August 2012, Second Deed of variation of Debenture dated 8th May 2014 and Third Deed of variation of Debenture dated 3rd April 2017 respectively and between **PRINCE AFRICA LIMITED OF P.O Box 5838 Dar es Salaam** (Borrower) and **I & M Bank (T) Limited** and every other power enabling me so to do, I **Annette W. Kirethi** being the Receiver/Manager of the entire charged assets, in Receivership hereby place the entire Borrower's assets for sale by way of tender.

2. Bidders are invited for the purchase of the following assets;

| Sn. | Assets | Quantity | Lot No. | Sn. | Assets | Quantity | Lot No. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Arun Mixer Machine Driven with 10HP motors | 2 | **2023-1** | 16. | Electrical LV PANEL Compressor and cooling system UTP with 4 Panel Treatment tank, filter system and dozing panel | 2 | **2023-16** |
| 2. | Compressor machine Model No. E18-10 Motor capacity:18.5kw Machine capacity:2.63m3 TS 10HN | 3 | **2023-2** | 17. | OMEGA 450 FERROMATIC MILACRON Operated by 103 HP motor. Produce 100 products per 1hr. yr. of mfg. 2008 | 2 | **2023-17** |
| 3. | Pu Chemical Machine Operated by 7HP motor machine | 2 | **2023-3** | 18. | OMEGA 775W FERROMATIC MILACRON Operated by 120 HP motor, produce 100 products per 1hr, yr of mfg. 2008 | 2 | **2023-18** |
| 4. | Punching machine Operated by 7HP motor machine | 1 | **2023-4** | 19. | OMEGA 660W FERROMATIC MILACRON Operated by 100 HP motor Produce 100 prod. per 1hr, yr. of mfg. 2008 | 1 | **2023-19** |
| 5. | Ice box mould Operated by 7HP motor machine | 5 | **2023-5** | 20. | Grinding Machine Operates by 7.5 HP motor machine serial No. 109330 | 1 | **2023-20** |
| 6. | HMP Tape filling machine Operated by 5HP motor machine | 1 | **2023-6** | 21. | Chiller Machine Connected with galvanised pipes, gate Valves, elbow joints and motors | 2 | **2023-21** |
| 7. | Crane Machine Capacity of tones 10 and 60 tonnes | 1 | **2023-7** | 22. | Plant Cooling System Machine is complete connected with galvanised pipes, gate valves, elbow joints and two motors with 20HP | 2 | **2023-22** |
| 8. | OMEGA 100 FERROMATIC MILACRON Operated by 38.5HP motor produce 100 products per 1 hour Yr. of mfg. 2008 | 1 | **2023-8** | 23. | Printing Machine Machine is complete connected with galvanised pipes, gate valves, elbow joints and two motors with 20HP | 2 | **2023-23** |
| 9. | OMEGA 350W FERROMATIC MILACRON Operated by 60HP motor produce 100 products per an hr. yr. of mfg. 2008 | 1 | **2023-9** | 24. | Screen Printing Machine It operates with 15HP motor | 1 | **2023-24** |
| 10. | OMEGA 200 W FERROMATIC MILACRON Operated by 55HP motor Produce products per 1hr, yr. of mfg. 2008 | 1 | **2023-10** | 25. | Air Receiver machine Connected with air pipes, gates valves, elbow joints and motor | 1 | **2023-25** |
| 11. | OMEGA 150W FERROMATIC MILACRON Operated by 55HP motor Produce 100 products per 1hr | 1 | **2023-11** | 26. | Drill Machine Operated by 15HP motor machine 3HPM | 1 | **2023-26** |
| 12. | Blow Moulding HC-90 HC-90 Model Operated by 90 HP motor Prod. 30 prod. per1hr. 2008 | 3 | **2023-12** | 27. | Welding Machine Serial No. WP, Capacity 400 AC, 80A/23.2 | 1 | **2023-27** |
| 13. | Grinding Machine Operated by 20HP motor | 5 | **2023-13** | 28. | Transformer Machine Serial No. W.P. Capacity 40 | 1 | **2023-28** |
| 14. | Various plastic printing moulds | 10 | **2023-14** | | | | |
| 15. | General office equipment Such as ACs, Generators, tables, chairs etc. | 5 | **2023-15** | | | | |

3. All the assets are located at Plot No.s 129 & 130 Block 216, Kipawa Industrial Area, Ilala Dar es Salaam.
4. Viewing dates for all bidders shall be conducted on 25th, 26th and 27th October 2023 between 14:00hrs-16:00hrs.
5. Each bid should be submitted in sealed envelopes with the specific lot number on the outside with a non-refundable fee of TZS. 100,000/= in bankers' cheque or cash indicating;
   (i) The identification of the assets i.e. lot no. and quantity proposed to be purchased
   (ii) The offer price for each asset bid for
   (iii) Full address and contact details of the bidder including contact telephone number and email address where possible. The bidder must inspect the assets and offer a price to purchase on the basis of that inspection only
6. The Assets shall be sold strictly on 'as is where is' basis.
7. The Purchased assets shall be removed from the site within fourteen (14) days from date of full payment of the purchase price at bidder's cost. Thereafter, there shall be a storage fee charged for each additional day of storage.
8. The Receiver/Manager is not bound to accept the highest bid or any bid at all.
9. The Receiver/Manager does not provide any warranty as to the condition of the equipment and machinery. Bidders are advised to inspect the equipment and seek professional opinion on the respective condition.
10. Any photograph and or description of the assets supplied herein are without liability of the Receiver/Manager as to their correctness. Independent valuation is strongly recommended.
11. The successful bidder shall be bound to pay 60% of the original purchase price within 7 days of being declared successful and the balance of 40% payment shall be paid in full and without deduction within 14 days from date of notification.
12. Should the successful bidder or intended purchaser fail to meet any of the terms of sale including but not limited to failure to pay the purchase price as provided above, the sale of such assets shall be cancelled and 10% of the bid amount ashall be forfeited.
13. **Deadline:**
Bids shall be submitted so as to reach the Receiver/Manager on the address below on or before **Tuesday 31st October 2023 at 16:00 hours**. Bids shall be opened at 16:30 hours thereafter at the Receiver/Manager's Offices. Successful bidders shall be notified within five days from the date of opening.

**BID ADDRESS**
Annette W. Kirethi
Receiver/Manager - Assets of Prince Africa Limited
C/O Hallmark Attorneys
18 Chole/Ruvu
Masaki Area
P.O. Box 13811
**Dar es Salaam**
Tel: 255 22 2124946/8
Email: info@hallmarkattorneys.co.tz;

**LATE SUBMISSIONS WILL BE DISREGARDED**

217666802

HABARI KITAIFA

# Dk. Mwinyi acharuka ujenzi holela

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameagiza mfumo wa ujenzi Unguja uhame kutoka makazi holela, sasa ni wakati wa kuufanya uwe wenye mwonekano mzuri.

Ni tamko lake la jana baada ya kuweka jiwe la msingi katika nyumba za makazi zilizoko Tomondo zinazojengwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) na nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba Zanzibar zilizoko Mombasa kwa Mchina, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema, moja ya ahadi katika Ilani ya CCM ya 2020/2025 ni kujenga nyumba za gharama nafuu kwa ajili ya wananchi.

Alisema serikali itaendeleza ujenzi wa nyumba hizo. Shirika la nyumba linaendelea na ujenzi wa nyumba ili wananchi wapate makazi bora.

Rais Dk. Mwinyi alisema serikali imeondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani katika ununuzi wa nyumba hizo ili kupunguza gharama na wananchi kupata unafuu wa kununua nyumba na kukaa katika makazi bora.

"Tutaendelea kupunguza kodi za nyumba hizo maana hapa tulipo watakaomudu ni wale wenye tabaka la kati, lakini wananchi wa kawaida hawatomudu nyumba hizi. Hilo litakua ni jukumu la serikali kuwa na nyumba za bei nafuu," alisema.

Aliwapongeza makandarasi kwa hatua nzuri za ujenzi wa nyumba hizo na kuridhika na hatua iliyofikiwa.

Aliwataka watakaokaa katika nyumba hizo kuzitunza kwa kuwa amebaini hakuna tabia ya utunzaji wa maeneo wanayoishi na ndio maana nyumba za maendeleo zilizojengwa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar ziko katika hali mbaya.

"Hatuna utamaduni wa kufanya ukarabati wa nyumba mara kwa mara. Tunasubiri mpaka nyumba inaanguka ndipo tunashtuka kuwa inahitaji matengenezo wakati nyumba hizo zikifanyiwa ukarabati wa mara kwa mara zina uwezo wa kudumu kwa muda mrefu," alisema.

"Fedha zote zilizokuwa zinapotea sasa zinarudi kwa maslahi ya nchi na leo hii kuna miradi mingi inafanyika na serikali ina uwezo wa kupandisha mishahara na pensheni jamii," alisema.

Aliongeza: "Maneno yanayosemwa katika mitandao, mimi kwangu hayaninyimi usingizi hata kidogo, kwa sababbu ninajua hoja zimetosha na hawana hoja nyingine. Wananchi waendelee kutuunga mkono katika kutekeleza miradi ya maendeleo."

Waziri wa Fedha, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema utekelezaji wa mradi huo ni maono ya Rais Dk. Mwinyi kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata makazi bora na salama.

"Wengi wao waliona kuwa hatutoweza kutekeleza maono ya Rais wa Kwanza Abeid Amani Karume lakini leo hii wewe Rais Dk. Mwinyi umeweza kutekeleza maono hayo ambapo mradi wa nyumba za ZSSF una nyumba 276," alibainisha.

Waziri huyo pia alisema miradi inayotekelezwa na mfuko huo imejikita katika kustawisha wanachama wake na kuona wanapata makazi bora zaidi wakati watakapostaafu utumishi wa serikali.

Alisema mradi wa nyumba za mkopo nafuu kwa wananchi wakiwamo wanachama wa ZSSF unatarajiwa kukamilika Machi mwakani. Nyumba 270 zitajengwa na kugawiwa kwa wananchi watakaozinunua.

Waziri wa Ardhi na Makazi, Rahma Kassim Ali, alisema maeneo kwa ajili ya miradi yapo na wizara yake itaendelea kujenga nyumba nyingi ili kuwapa nafuu ya makazi wananchi wa Zanzibar.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Mohamed Said Dimwa, alisema chama kimefurahishwa na kasi ya utekelezaji wa ilani yao ya uchaguzi katika kuleta maendeleo kwa wananchi.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akifungua pazia kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa nyumba za gharama nafuu za Mji wa Dk. Hussein Mwinyi Tomondo, Wilaya ya Magharibi "B", Mkoa wa Mjini Magharibi jana, akiwa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo mkoani humo katika shamra shamra za kutimiza miaka mitatu ya uongozi wake. Kushoto ni Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Mohamed Said Dimwa na Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum. **PICHA: IKULU**

# NECTA yaonya udanganyifu mitihani la IV, kidato cha II

**Na Romana Mallya**

UPIMAJI Kitaifa wa Darasa la Nne 2023 unaanza leo ukihusisha wanafunzi 1,692,802 waliosajiliwa, huku Baraza la Mitihani (NECTA) likionya wadau wakiwamo wasimamizi wa mtihani, wanafunzi, wazazi na wamiliki wa shule dhidi ya udanganyifu.

Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Dk. Said Mohamed, akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za baraza mkoani Dar es Salaam jana, alisema mtihani huo utafanyika kwa siku mbili na kuhusisha shule za msingi 19,284 Tanzania Bara.

Vilevile, alisema kwa siku 11 kutafanyika Mtihani wa Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) ambao utafanyika katika shule za sekondari 5,546 Tanzania Bara. Kuhusu Upimaji Kitaifa Darasa la Nne, Dk. Mohamed alisema kati ya wanafunzi 1,692,802 waliosajiliwa kuufanya, wavulana ni 828,591 sawa na asilimia 48.95 na wasichana ni 864,211 sawa na asilimia 51.05.

Alisema, wanafunzi 1,605,379 sawa na asilimia 94.84 watafanya upimaji kwa lugha ya Kiswahili na wanafunzi 87,423 sawa na asilimia 5.16 wataufanya kwa lugha ya Kiingereza ambayo wamekuwa wanaitumia katika kujifunza.

Katibu Mtendaji huyo alisema wanafunzi wenye mahitaji maalum wako 6,402. Kati yao, 1,074 ni wenye uoni hafifu, 93 ni wasioona, 1,240 wenye ulemavu wa kusikia, 2,209 ni wenye mtindio wa akili na 1,786 ni wenye ulemavu wa viungo vya mwili.

Dk. Mohamed alisema wanafunzi 759,573 wamesajiliwa katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili 2023. Kati yao, wavulana ni 353,807 sawa na asilimia 46.58 na wasichana ni 405,766 sawa na asilimia 53.42.

"Wanafunzi wenye mahitaji maalum wako 1,382. Kati yao, 683 ni wenye uoni hafifu, 82 ni wasioona, 290 wenye ulemavu wa kusikia na 309 ni wenye ulemavu wa viungo vya mwili na 18 wenye ulemavu wa akili," alifafanua.

Dk. Mohamed alisema maandalizi yote kwa ajili ya upimaji huo yamekamilika ikiwa ni pamoja na kusambazwa kwa karatasi za upimaji na nyaraka zote muhimu zinazohusu mitihani hiyo.

Alisema, baraza linatoa wito kwa wasimamizi wote walioteuliwa kusimamia upimaji, kufanya kazi yao ya usimamizi kwa umakini na uadilifu wa hali ya juu.

"Baraza linaamini kuwa walimu wamewaandaa wanafunzi vizuri katika kipindi chote cha miaka miwili. Ni matarajio ya baraza kuwa wanafunzi watafanya upimaji kwa kuzingatia kanuni za mitihani.

"Baraza halitarajii kuona mwanafunzi yeyote kujihusisha na vitendo vya udanganyifu, atakayebainika matokeo yake yatafutwa kwa mujibu wa kanuni za mitihani," alisema.

Dk. Mohamed alitoa wito kwa wamiliki wa shule kutambua kuwa shule zao ni vituo maalum vya mitihani, hivyo halitasita kukifuta kituo chochote endapo litajiridhisha pasipo shaka kuwapo kwake kunahatarisha usalama wa upimaji wa kitaifa.

Alitoa rai kwa jamii kulipa ushirikiano baraza katika kuhakikisha upimaji wa darasa la nne na kidato cha pili unafanyika kwa amani na utulivu.

"Baraza linaomba wananchi kutoa ushirikiano wakati wote wa uendeshaji upimaji ili wanafunzi wote wafanye upimaji katika hali ya utulivu na katika kudhibiti vitendo vyovyote vya udanganyifu," alisema.

## Hospitali yapima haja kubwa kugundua TB

**Na Cleopatra Mokiwa**

KIFUA kikuu (TB) ni moja ya magonjwa hatari. Unasababishwa na vimelea aina ya Mycobacterium Tuberculosis visivyoonekana kwa macho. Ni lazima utumie hadubini.

Ni ugonjwa ambao umekuwa tishio kwa jamii kwa miongo kadhaa. Unaathiri mapafu na sehemu nyingine za mwili na mara nyingi huchukua muda mrefu kugundulika kutokana na uelewa mdogo katika jamii, hivyo kuchelewa kugundua tatizo mapema.

TB inagunduliwa kwa njia ya upimaji wa makohozi kwa njia ya hadubini na vinasaba (Gene xpert) vipimo hivi ni Bure.

Hata hivyo, Wizara ya Afya kupitia Mpango wa Kutokomeza Kifua Kikuu, imeongeza kipimo kingine cha ugunduzi wa TB kwa kutumia haja kubwa kwa makundi maalum ambayo ni watoto wenye umri chini ya miaka tano ambao hawana uwezo wa kutoa sampuli ya makohozi, wagonjwa wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na wagonjwa waliolala kitandani muda mrefu waliozidiwa.

Hospitali ya Rufani ya Mkoa Temeke (TRRH) imeanza kutoa huduma za kiuchunguzi kwa wahisiwa wa kifua kikuu kupitia kipimo hicho kipya. Kinatumia vinasaba (Stool for Gene xpert) na kufanikiwa kugundua wagonjwa kadhaa ikiwamo mtoto wa miezi mitano.

Dk. Rose Chagama, mtaalamu wa kifua kikuu na ukoma katika hospitali hiyo, anaeleza kuwa kipimo hicho ni kipya kwa Tanzania na kwa Hospitali ya Temeke huduma imeanza kutolewa mwishoni mwa mwezi uliopita. Kipimo hicho ni mahususi kwa makundi maalum.

"Ni kipimo kipya kwa Tanzania na kilifanyiwa utafiti maeneo kadhaa na kuthibitishwa kuwa kinafaa kutumika sasa. Wizara imeruhusu kitumike, hivyo kwetu hapa Temeke huduma hii imeanza mwezi wa tisa (Septemba) mwaka huu.

"Kipimo hiki ni kwa wale wahisiwa (presumptive) wa kifua kikuu, ambao wako katika makundi maalam kama vile watoto waliopo chini ya miaka mitano ambao hawawezi kutoa makohozi, wagonjwa waishio na VVU pamoja na wale walioumwa muda mrefu na wako vitandani hawajiwezi," anafafanua.

Kupitia kipimo hicho, Dk. Rose anasema ufanisi utaongezeka katika utoaji huduma na kupunguza vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano na kwa wagonjwa wanaoishi na VVU kwa kuwa TB ni moja ya magonjwa nyemelezi yanayowapata na wengi kupoteza maisha.

## TANGAZO

# TAARIFA YA VIWANGO VYA TIGO KWA ROBO YA TATU (JULAI - SEPTEMBA 2023)

### Viwango unavyotozwa kadri unavyotumia (Na Kodi)

** - Malipo ya sauti yamekadiriwa kwenye sekunde iliyo karibu
- Malipo ya data yamekadiriwa kwa shilingi 0.09 kwa kila kilobaiti 10 za data

**VIWANGO VYA NDANI**

| Aina za simu | Bei (TSh/Dk) |
|---|---|
| Tigo - Tigo (Viwango ni vya muda wowote) | 30 |
| Tigo - Mitandao mingine (Viwango ni vya muda wowote) | 30 |

**VIWANGO VYA KIMATAIFA - TIGO**

| Aina za simu (Kanda/Makundi) | Bei (TSh/Dk) | Nchi |
|---|---|---|
| Kundi 1 | 720 | China, India, Marekani, Canada |
| Kundi 2 | 1020 | Kenya, Angola, Afrika Kusini, Nigeria, Botswana, Ghana, Ethiopia |
| Kundi 3 | 1020 | Lebanon, Israeli, Hispania, Falme za Kiarabu, Uingereza (simu za kiganjani), Uingereza (Simu za mezani) |
| Kundi 4 | 1200 | Sweden, Hong Kong, Pakistani, Yemen, Ufilipino, Saudi Arabia, Uholanzi, Japan, Malaysia, Norway, Ireland |
| Kundi 5 | 1800 | Australia, Nepal, Uturuki, Urusi, Visiwa vya Comoro, Uganda, Rwanda, Ufaransa, Denmark, Italia, Oman, Ujerumani |
| Kundi 6 | 2520 | Nchi nyinginezo |
| Kundi 7 | 2520 | Cuba, DRC, Burundi, Zimbabwe, Msumbiji, Uswisi, Malawi, Zambia |
| Kundi 8 | 19800 | Mitandao yote ya satelaiti |

**VIWANGO VYA KIMATAIFA - ZANTEL**

| Aina za simu (Kanda/Makundi) | Bei (TSh/Dk) | Nchi |
|---|---|---|
| Kundi 1 | 497 | Marekani, India, China, Canada |
| Kundi 2 | 1020 | Kenya, Falme za Kiarabu, Afrika Kusini, Denmark, Sweden, Norway, Ireland, Uingereza (simu za kiganjani), Uingereza (Simu za mezani), Hispania, Ufaransa, Italia, Pakistani, Zimbabwe, Ujerumani |
| Kundi 3 | 1325 | DRC, Yemen, Omani, Lebanon, Israel, Sudani |
| Kundi 4 | 1500 | Zimbabwe (simu za kiganjani), Msumbiji, Malawi, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia, Mayote, Sudani ya Kusini |
| Kundi 5 | 1200 | Nchi nyinginezo |
| Kundi 6 | 3000 | Cuba, Vanuatu, Tunisia, Tonga (simu za kiganjani), Tokelau, Uswisi, Somalia,Visiwa vya Shelisheli, Nauru, Samoa, Madagascar, Slovenia, Visiwa vya Comoro |
| Special | 18000 | Mitandao yote ya satelaiti |

**VIWANGO VYA SMS**

| Aina za SMS | Bei (TSh/SMS) |
|---|---|
| SMS za kitaifa | 8 |
| SMS za kimataifa | 215 |

**VIWANGO VYA DATA**

| Intaneti | Bei (TSh) |
|---|---|
| Data kwa MB | 9.35 |

### VIWANGO VYA VIFURUSHI VYA DAKIKA, INTANETI NA SMS (Na Kodi)

**MITANDAO YOTE**

| Bei (TSh) | Dakika za Tigo-Tigo / Zantel-Zantel | Dakika za Mitandao yote | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 500 | 90 | 10 | 100 | 25 | 0 | Saa 24 |
| 500 | 0 | 30 | 30 | 25 | 10 | Saa 24 |
| 1000 | 0 | 150 | 150 | 25 | 0 | Saa 48 |
| 1500 | 0 | 180 | 180 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 1500 | 250 | 50 | 300 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 2000 | 0 | 250 | 250 | 100 | 50 | Siku 7 |
| 3000 | 0 | 450 | 450 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 3000 | 55 | 70 | 125 | 50 | 1024 | Siku 7 |
| 5000 | 100 | 180 | 280 | 100 | 1434 | Siku 7 |
| 5000 | 0 | 400 | 400 | 100 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | 0 | 1200 | 1200 | 100 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | 0 | 500 | 500 | 50 | 3072 | Siku 30 |
| 20000 | 0 | 800 | 800 | 50 | 7168 | Siku 30 |
| 30000 | 0 | 900 | 900 | 500 | 11264 | Siku 30 |

**SMS**

| Bei (TSh) | Dakika za Tigo-Tigo / Zantel-Zantel | Dakika za Mitandao yote | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 200 | 0 | 0 | 0 | 200 | 0 | Saa 24 |
| 500 | 0 | 0 | 0 | 1000 | 0 | Siku 7 |
| 1000 | 0 | 0 | 0 | 10000 | 0 | Siku 30 |

**BILA KIKOMO**

| Bei (TSh) | Dakika za Tigo-Tigo / Zantel-Zantel | Dakika za Mitandao yote | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1000 | 0 | 30 | 30 | 50 | 0 | Bila Kikomo |
| 1000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 250 | Bila Kikomo |

**INTANETI**

| Bei (TSh) | MB | Muda | Ziada |
|---|---|---|---|
| 500 | 246 | 24 hrs | N/A |
| 1000 | 492 | 24 hrs | N/A |
| 2000 | 985 | 24 hrs | N/A |
| 2000 | 950 | 7 days | N/A |
| 2100 | 1024 | 7 days | N/A |
| 3000 | 1434 | 7 days | N/A |
| 5000 | 2458 | 7 days | N/A |
| 10000 | 4920 | 7 days | N/A |
| 15000 | 7373 | 7 days | N/A |
| 10000 | 4920 | 30 days | N/A |
| 20000 | 9830 | 30 days | N/A |
| 35000 | 17240 | 30 days | N/A |
| 50000 | 24576 | 60 days | N/A |
| 100000 | 49152 | 60 days | N/A |

**KIMATAIFA - TIGO**

| Bei (TSh) | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 10 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 40 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Nigeria,Ghana - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Misri - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Omani, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Ufaransa - Dk 4 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 80 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Omani, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Nigeria,Ghana - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Misri - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Algeria, Morocco, Tunisia - Dk 5 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 12 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Nigeria,Ghana - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Misri - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 180 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Omani, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 18 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Ufaransa - Dk 13 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Nigeria, Ghana - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Misri - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 24 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Oman, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 38 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Algeria, Morocco, Tunisia - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |

**KIMATAIFA - ZANTEL**

| Bei (TSh) | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1000 | China, India - Dk 22 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 1000 | Marekani, Canada - Dk 25 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Afrika Kusini, Mauritius - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon, Yemen, Sudan, Misri - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Oman - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Pakistani, Hong Kong, Japan - Dk 10 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Ufaransa - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Ujerumani, Italia, Uingereza (simu za mezani), Uturuki - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Kenya, Uganda, Rwanda - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msumbiji - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Afrika Kusini, Mauritius - Dk 11 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon, Yemen, Sudan, Misri - Dk 11 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Oman - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Ufaransa - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | China, India - Dk 110 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Marekani, Canada - Dk 110 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Pakistani, Hong Kong, Japan - Dk 25 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 7500 | Ujerumani, Italia, Uingereza (simu za mezani), Uturuki - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 7500 | Kenya, Uganda, Rwanda - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |

**HONORA TANZANIA PLC,**
PSSSF Commercial Complex, Kiwanja Na. 24, Kitalu Na. 3, Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P. 2929, Dar es Salaam, Tanzania.

www.tigo.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mpango wa kuwekeza katika hospitali utaimarisha huduma

**SERIKALI** ya Zanzibar imeamua kuwekeza katika huduma ya afya kwa kujenga hospitali ya wilaya na kuiweka katika mfumo binafsi, ili kupata ufanisi katika uendeshaji wake.

Utaratibu huo kwa mujibu wa Rais wa Zanzibar, Hussein Ali Mwinyi, utasaidia kupunguzia mzigo hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo hata wagonjwa wanaougua maradhi yanayohitaji hospitali ndogo hukimbilia huko.

Hospitali ya Wilaya ya Kaskazini A Unguja ni miongoni mwa zilizojengwa kupitia fedha za Mpango wa Kukabiliana na Athari za UVIKO-19 zilizotolewa kupitia mkopo wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

Lengo la Serikali ya Zanzibar ni kuona kuwa huduma za afya hazidorori baada ya kushirikisha sekta binafsi.

Mara kadhaa inatokea katika hospitali za serikali ambapo kifaa kikiharibika, utaratibu wa serikali unataka ufuate sheria ya ununuzi na huchukua muda mrefu hadi kukamilika na huwaumiza watu, kwa sababu hakuna mgonjwa anayeweza kusubiri mpaka utaratibu wa ununuzi ukamilike.

Kwetu sisi tunasema utaratibu huu ni mzuri na utasaidia kuboresha huduma katika sekta ya afya na kuondoa malalamiko kutoka kwa wananchi.

Ni kweli wagonjwa wengi wanateseka wanapokwenda kwenye hospitali za serikali kufuata tiba ambazo huduma zake ni nafuu na kuambiwa kuwa kipimo fulani hawezi kukipata kwa kuwa kifaa kimeharibika mpaka kitakapopatikana kingine.

Ugonjwa hauwezi kusubiri kifaa kingine kinunuliwe hivyo, mbadala ni kwenda hospitali za binafsi ambazo vifaa hivyo hupatikana, lakini kwa gharama ya juu.

Serikali inapoamua kujenga hospitali na kuamua iendeshwe katika mfumo wa ubinafsishaji kutaboresha ufanisi na wananchi kupata huduma ya uhakika.

Utaratibu huu pia ungefanyika katika huduma zingine zinazotolewa na taasisi za serikali kwa kubinafsishwa ili kuongeza kasi ya ufanisi na kuleta tija katika utoaji huduma.

Wafanyakazi wanaofanyakazi katika taasisi za serikali, baadhi yao hujisahau na kutekeleza wajibu wao kwa mazoea.

Kama utaratibu ulivyofanywa kwenye hospitali hiyo ya wilaya basi ufanyike kwenye taasisi zingine ili kuleta ushindani katika kutoa huduma na kuboresha huduma.

Pia, Rais Mwinyi aliagiza kwa huduma ambazo si za kitalaam, ikiwamo usafi wa hospitali wachukuliwe vijana wazawa wafanye kazi hiyo ili kusaidia kutatua tatizo la ajira ambalo linaikabili taifa kwa sasa.

Utaratibu wa kubinafsisha hospitali hiyo kwa mujibu wa Rais Mwinyi una dhamira njema ya kufanya huduma za afya kuwa bora zaidi na zenye kuleta ufanisi.

Katika mabadiliko yoyote lazima kutakuwa na hofu ya ajira kwa wale waliopo kazini kupoteza nafasi zao, lakini katika hilo Rais Mwinyi aliwaondoa hofu, lakini akawataka kujifunza ujuzi utakaotolewa na madaktari watakaokwenda kuboresha huduma za afya.

Faida ya kufanyakazi na watalaam ambao wametoka sehemu nyingine, unajifunza kile ambacho hukuwa unakijua na wewe unaongeza maarifa na ujuzi.

Ndio maana serikali mara kwa mara inakaribisha wataalam kutoka nchi zingine kuja Tanzania kushirikiana na wataalam wa nchini ili ujuzi watakaoupata kutoka kwao waweze kuutumia kuboresha huduma ya afya nchini.

Hospitali hiyo ya Wilaya ya Kaskazini Unguja, iwe mfano kwa nyingine ili kuleta ufanisi katika sekta ya afya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Karibu DP World tujifunze kwako

**UWEKEZAJI** wa bandari ya Dar es Salaam, umefanyika na wananchi wamesikia baada ya kuelezwa mafanikio yanayotarajiwa kupatikana pamoja na ongezeko la mapato ya taifa .

Lilikuwa suala lililozua mjadala mkubwa kwa sababu Watanzania kwa miaka mingi wamekuwa wakilalamikia matokeo kwenye mikataba ya uwekezaji kwa sababu walihisi hakuna fursa wala faida zilizopatikana.

Ni wazi kuwa wananchi hawapingi uwekezaji huo lakini walikuwa na hofu kutokana na upungufu wanaouona hasa kwenye sekta za madini, viwanda vilivyobinafsishwa, mashirika ya umma kama reli na ndege na kuzidi kuamini kuwa pengine kuna walakini kwenye ubinafsishaji, ukodishwaji na ubia au ushirikiano kwenye kuendesha mashirika ya umma.

Wakati mkataba unapozainiwa wanaelezwa kuwa mwaka 2021/22 TRA ilikusanya Shilingi trilioni 7.8 lakini ujio wa uwekezaji utapandisha kiwango hicho hadi kufikia trilioni 26.7 ifikapo 2032/33.

Wanahakikishiwa kuwa zipo fursa nyingi za kiuchumi ambazo zipo kwenye ushirikiano huo wa kiuchumi ikiwa ni pamoja na bandari ya Dar es Salaam, kupokea shehena zaidi, kiufanisi na kwa kuaminiwa na kuhudumia mataifa yasiyo na bahari yanayoizunguka Tanzania.

Mkataba mpya wa uwekezaji wa bandari unatajwa kuwa na fursa na faida zake mfano ni mkakati wa kiuchumi unaoshirikisha wawekezaji wa nje na ndani.

Vilevile ni kujenga uchumi ambao serikali inawekeza moja kwa moja kwa kushirikiana na sekta binafsi siyo kuachia kampuni binafsi pekee.

Ni ukweli kuwa bandari za Dar-es Salaam,Tanga na Mtwara bado ufanisi wake wa kuhudumia shehena uko chini kwa kulinganisha na mahitaji ya kusafirisha,kuhifadhi, kupakua na kuhudumia mizigo inayotoka na kwenda Rwanda, Burundi, Congo DRC, Malawi, Zambia na hata Zimbabwe.

Ni wazi uwekezaji wa bandari ya Dar es Salaam unahitaji kuboreshwa ili kuwa na mifumo na vifaa vya kisasa pengine huenda walivyoko TPA haviendani na ulimwengu wa sasa hasa unaohakikishia shehena zinakuwa salama kuanzia zinapopakiwa hadi kupokelewa na kufikishwa kwa wateja.

Kwa ujumla, serikali iliona kuwa ni vyema kupata mwekezaji atakayewekeza kwa mifumo ya kisasa na kwa faida.

Hata hivyo ni vyema kwa watumishi wanaofanya kazi na mwekezaji DP World kuwa na uadilifu na uaminifu kwa taifa lao ili matamanio hayo ya serikali na Watanzania yafikiwe.

Uwekezaji huo uwe darasa ili kuwaanda wataalamu watakaokuwa wamepikwa na kuelewa kikamilifu jinsi ya kuzihudumia bandari za Tanga, Mtwara , Bagamoyo na zile za maziwa.

Ni kwa sababu dunia ya leo kila jambo ni kujifunza kupitia uhawilishaji wa teknolojia na maarifa kutoka kwa wabobezi kwenda kwa wale waoakua kiuchumi.

Ni wazi kuwa ufanisi wa kampuni ya DP World haukushushwa kutoka juu ila ni juhudi na uwekezaji kuanzia rasilimali, watumishi, mafunzo, miundombinu, utafiti, sheria na kufuata maelekezo na uwajibikaji.

Ikiwa hayo ni sehemu ya mafanikio yao, Tanzania nayo ina nafasi ya kujifunza na kuzifahamu mbinu za kuongeza ufanisi , ikiwa DP World itaongeza kiwango cha shehema inayopitishwa Dar-es Salaam kutoka tani milioni nane za sasa kwa mwaka hadi zifikie milioni 60, Watanzania wana mengi ya kujifunza na kugundua.

Bandari hiyo ni lango kuu linaloingiza shehena kubwa hivyo juhudi zilizotumiwa kuwaelimisha wananchi wakaufahamu ukweli huo, zitumike kuwafahamisha faida za uwekezaji huo mkubwa unaofungua milango ya biashara.

Baada ya Watanzania kuelezwa na kufahamishwa kuhusu uwekezaji wa mkataba huo wameamini kuwa chombo hicho cha biashara na uchumi, pamoja na uwekezaji hakijauzwa na kwamba mamlaka yake iko kwenye ulinzi na usalama wa nchi , hivyo ni wakati wa kuona uingizaji bidhaa ukiimarika na pwani ikiwa na ulinzi madhubuti.

Taifa litarajie kuona ulinzi na usimamizi ukiimarika na kuondoa bandari bubu zinazoingiza dawa za kulevya, bidhaa duni, hatarishi, feki tena zilizokwepa ushuru, wahalifu na kutishia hatama ya uwekezaji huo unaolipa taifa matumaini makubwa ya kupata mafanikio.

HABARI KITAIFA

MAUAJI YA ANETH MSUYA

# Mke wa Bilionea Msuya akana alichokiri Polisi

**Na Grace Gurisha**

MIRIAM Mrita, aliyekuwa mke wa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha, marehemu Erasto Msuya 'Bilionea Msuya', amedai mahakamani kuwa alikaa siku tatu bila kula wala kunywa huku akishinikizwa na askari polisi kukiri kumuua wifi yake, Aneth Msuya.

Pia, amedai alikaa kwenye chumba usiku kucha akiwa amefungwa kitambaa cheusi usoni na pingu mikononi na kwa kipindi chote hicho tangu akamatwe Agosti 5, 2016, ndugu, jamaa na marafiki hawakujua alikokuwa.

Mrita alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akitoa utetezi wake katika kesi ya mauaji inayomkabili na mfanyabiashara Revocatus Muyela, wote wakazi wa Arusha wanaotuhumiwa kumuua Aneth.

Akiongozwa na Wakili wa wake, Peter Kibatala, Mrita alidai anakumbuka alikamatwa tarehe hiyo akiwa katika Klabu ya Tembo mkoani Arusha. Akiwa anakula chakula, aliwekwa chini ya ulinzi na Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, SSP David Mhanaya aliyekuwa na askari wengine, akiwamo Latifa Chiku.

"Wakati nipo kwenye meza, David Mhanaya aliwahi kuchukua simu yangu mezani na WP Latifa alichukua pochi yangu ambayo ndani kulikuwa na Dola za Marekani 500, Sh. 600,000, simu mbili, perfume (manukato) mbili na pasipoti hadi leo hii ninajitetea, sijawahi kupewa hivi vitu vyangu," alidai Mrita.

Alidai kuwa SSP Mhanaya pamoja na askari hao (Jumanne Malangai na Latifa Chiku) walimchukua hadi Kituo Kikuu cha Polisi Arusha na alipohoji kosa la kushikiliwa kwake, Afande Mhanaya alimweleza "utafahamu hayo huko mbele".

Mrita alidai kuwa alipofika kituo cha polisi aliingizwa ndani na Afande Mhanaya, alimtambulisha kwa mtu kwamba ni Mkuu wa Kituo hicho, hivyo azungumze naye, alimwuliza kama anamfahamu Gadi Solomoni, Israeli Solomoni, akajibu anawafahamu ni shemeji zake.

"Aliniuliza tena kama ninamfahamu Elisalia Msuya nikamjibu kuwa 'ni baba mkwe wangu' na aliponitajia Ndeshukulwa nilimweleza kuwa 'ni mama mkwe wangu', akaniuliza 'na Claudia unamfahamu? Nikamjibu 'ndiyo namfahamu ni mchimbaji Tanzanite One'," alidai Mrita.

Alidai kuwa baada ya hapo walimwamuru apande kwenye gari, awapeleke nyumbani kwake wakafanye upekuzi. Katika upekuzi huo Afande Mhanaya alimweleza kwamba amwoneshe cheni za dhahabu ambazo alikuwa anamringishia mama mkwe wake.

Mrita alidai kuwa alishangaa kwa hilo, akamjibu kwa kumhoji 'kwani mama mkwe ni mke mwenzangu hadi niling-ishie hizo dhahabu?' Wakati yeye anakaa Arusha, mama mkwe alikuwa anaishi Mirerani.

"Afande Mhanaya akaniambia 'usijifanye wewe ndiyo msimamizi wa mirathi, mirathi inaweza kusimamiwa na bibi, babu hata mjomba'. Hadi muda huo hakuna askari aliyeniambia nina tuhuma na kesi ya mauaji ya Aneth," alidai.

Mshtakiwa huyo alidai kuwa walipomaliza upekuzi, walirejea Kituo Kikuu cha Polisi Arusha na kuanza safari ya kwenda Dar es Salaam. Walipokuwa njiani, gari aina ya landcruser lilibadilishwa namba mara mbili na walipofika njia ya Chalinze na Bagamoyo walipaki gari pembeni, wakamwamuru apande gari lingine lililokuwa nyuma yao.

"Tulipofika maeneo ya Tegeta, Afande Mhanaya alimwonesha kwa ishara Afande Latifah, akaniambia nigeuke upande wangu wa kushoto na akanifunga kitambaa usoni. Baada ya kufunguliwa macho, nikaona chumba chenye grili nikaingizwa humo," alidai.

Mshtakiwa huyo alidai kuwa baada ya kufika eneo hilo ambalo hajui kama ni Kituo cha Polisi au la, alibadilishwa kwenye vyumba mara nane kuanzia Agosti 6, 2016 hadi Agosti 8, 2016.

"Agosti 6, 2016 nilifungwa kitambaa usoni na kufungwa pingu mikononi hadi Agosti 7, 2016. Wakati Afande Latifa anaondoka, nikamwuliza swali 'unaponifunga hivi unataka nijisaidi-aje?' Akaniambia hayo ndiyo malipo ya muuaji na ilipofika usiku wa manane nilipiga kelele.

"Alipopita afande nikamwomba anifungue pingu ili niende kujisaidia, alinijibu kwamba walionifunga wameondoka na funguo ya pingu," alidai.

Mrita alidai alijua kuwa ni asubuhi baada ya kufunguliwa kitambaa na Afande Latifa aliyemtaka amfuate alikokuwa anelekea.

"Nilifungwa tena kitambaa nikapelekwa kwenye chumba kingine ambako nilipewa kikombe cha chai ya rangi na maandazi mawili, nikaamuliwa nile, tangu nikamtwe ndipo nimekuja kunywa chai tarehe saba, siku zote hizo sikuwa nimekula wala kunywa," alidai.

Alidai kuwa Afande Mhanaya alimwuliza kama ana shida yoyote ya kiafya akamweleza kwamba yeye amejifungua kwa operesheni ndipo alipomtaka Latifa amkague. Alimtaka alale chini chali ili akaguliwe wakati anafunuliwa kukaguliwa, Afande Mhanaya hakutoka eneo hilo na alipewa jibu kuwa ni kweli ana mshono.

Mshtakiwa huyo aliendelea kudai mahakamani kuwa alikumbana na mateso kwa kupigwa na kitu kizito kwenye miguu hadi kushindwa kutembea na siku anapandishwa kizimbani kwa mara ya kwanza Agosti 23, 2016 alikuwa hawezi kutembea vizuri.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi leo kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa upande wa utetezi. Upande wa Jamhuri unawakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Paul Kimweri, Yasinta Peter, Generosa Montana na Marietha Maguta.

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo ya mauaji ya wifi yake, Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa kukiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo.



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga (wa pili kulia), akikabidhi tuzo kwa Mkurugenzi wa Kituo cha Mafuta cha Puma Arusha, Husin Sjat baada ya kuibuka mshindi wa kwanza wa tuzo za watoa huduma wa Puma Energy Tanzania mwaka 2023, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Puma, Dk. Seleman Majige (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Tanzania, Fatma Abdallah. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jela maisha kubaka kwa makundi

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, imewahukumu wakazi wawili wa Kijiji cha Mihumo Darajani, kifungo cha maisha gerezani, baada ya kupatikana na kosa la kumbaka kwa makundi msichana mwenye umri wa miaka 19.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Christopher Makwaya, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka, ikiwa ni pamoja na washtakiwa kukiri kosa.

Washtakiwa hao, Tamimu Mpoto (20) na Azizi Mkungura (27), walipoulizwa na Hakimu Makwaya kama wana sababu za msingi zitakazoishawishi mahakama isiwape adhabu kali, kila mmoja kwa wakati tofauti aliiomba mahakama iwaonee huruma kutowapa adhabu kali kwa kuwa wana wazazi wanaowategemea.

Washtakiwa walidai walilazimika kufanya kosa hilo, baada ya kutingwa na ibilisi wa mapenzi na kujikuta wakinasa kufanya unyama huo.

Kutokana na utetezi huo, Hakimu Makwaya alimuuliza Mwendesha Mashtaka wa Serikali Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Kibwana Kizulege, kama ana kumbukumbu za makosa ya zamani kwa washtakiwa hao na kujibu hana, huku akiomba kuwapa adhabu kali, iwe fundisho kwao na wengine wenye tabia kama hiyo.

Hakimu Makwaya akitoa hukumu, alisema anakubaliana na ombi la mwendesha mashtaka wa serikali na kutupilia mbali utetezi wao na kuwahukumu kila mmoja kifungo cha maisha gerezani.

Awali, ilidaiwa na mwendesha mashtaka kwamba washtakiwa walifanya unyama huo Kijiji cha Mihumo, Aprili 13, mwaka huu, baada ya kumrubuni msichana huyo kumuhitaji kwenda nyumbani kwa mmoja wao ambaye alikuwa mpenzi wake kwa ajili ya kutekeleza kile wanachokitekeleza siku zote.

Mwendesa mashtaka huyo alidai baada ya msichana huyo kuwasili nyumbani kwa mpenzi wake alijikuta akivamiwa na kundi la wanaume zaidi ya kumi na kumbaka hadi alipofanikiwa kujiokoa na kukimbilia kituo cha polisi kutoa taarifa unyama aliofanyiwa.

KABWELA — FADHILI MOHAMED



# Uzinduzi wa majadiliano kibiashara Marekani na Tanzania

●Ufunguo wa biashara na ustawi wenye manufaa

**Na Balozi Michael A. Battle Sr.**

ALHAMISI iliyopita, Marekani na Tanzania zimeingia katika ukurasa mpya wa kimageuzi katika ushirikiano, ambao Waziri wa Biashara wa Marekani Gina Raimondo na Waziri wa Viwanda na Biashara wa Tanzania, Dk. Ashatu Kijaji, wamesaini hati ya makubaliano ya kuwa na majadiliano ya kibiashara kati ya Marekani na Tanzania. Makubaliano hayo ya kihistoria yanatokana na ziara yenye mafanikio makubwa ya Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris nchini Tanzania, mwanzoni mwa mwaka huu, ziara iliyoweka msingi wa kuinua ukuzaji uchumi, uwekezaji, biashara na ustawi baina ya nchi hizo mbili.

Kusainiwa kwa makubaliano hayo kunakuja katika kipindi muhimu katika uhusiano rasmi na kunaimarisha dhamira ya dhati ya kufanya kazi pamoja ili kuimarisha uhusiano wa kiuchumi kama wabia katika misingi ya kuheshimiana na maadili ya pamoja.

Marekani na Tanzania zinaingia katika zama mpya, ambazo zinatekeleza vipaumbele vya ushirikiano wa maendeleo wakati huo huo ikiweka msisitizo zaidi katika kuimarisha uwekezaji na uhusiano wa kibiashara baina ya nchi hizo mbili.

Serikali ya Marekani na wawekezaji wake wanakuja Tanzania, wakiwa tayari kushirikiana kwa namna ambayo itafungua uwezo na fursa kubwa ya kiuchumi ya Tanzania, inayothibitishwa na utajiri wake mkubwa wa rasilimali watu na maliasili zake nyingi.

Marekani inataka msingi na wigo wa kiuchumi wa Tanzania ukue, na inaamini katika uwezo wake wa kukua. Majadiliano ya Kibiashara kati ya Marekani na Tanzania ni kielelezo muhimu cha dhamira ya dhati katika kufikia lengo hilo.

Yatakapotekelezwa, makubaliano hayo yatakuwa chachu ya kuongeza biashara kati ya Marekani na Tanzania kwa namna ambayo itawanufaisha moja kwa moja watu wa Tanzania.

Wafanyabiashara wa Marekani tayari wanawekeza katika sekta muhimu za uchumi wa Tanzania, lakini hivi sasa uhusiano wa kiuchumi unaelekea kupaa zaidi. Uhusiano wa kibiashara kati ya Marekani na Tanzania ni imara, lakini pia kuna mengi ya kuyafanyia kazi ili uweze kukua zaidi.

Mafanikio yaliyofikiwa hivi karibuni kama vile kampuni ya Ward Holdings kuweza kutuma shehena ya korosho zilizobanguliwa katika soko la Marekani, kupokelewa kwa ndege za Boeing kwa ajili ya Air Tanzania, na maendeleo yaliyofikiwa katika kuchakata madini ya nickel hadi kufikia kiwango kinachoweza kutumiwa kuzalisha betri kwa ajili kutumika katika teknolojia ya nishati safi ni maendeleo makubwa sana. Kwa kusaini makubaliano ya Majadiliano ya Kibiashara kati ya Marekani na Tanzania, kwa pamoja, tunapiga hatua nyingine kubwa katika kufikia kikamilifu uwezo huo.

Kwamujibu wa makubaliano hayo, majadiliano ya kibiashara yataongozwa kwa pamoja na Waziri wa Viwanda na Biashara wa Tanzania na Waziri wa Biashara wa Marekani. Nchi hizo zitapokezana katika kuandaa mikutano ya kila mwaka ambayo washiriki wake watajumuisha maofisa waandamizi wa serikali za Marekani na Tanzania na viongozi wakuu wa wadau wa sekta binafsi. Katikati ya kila mkutano wa mwaka, wawakilishi wa Ubalozi wa Marekani jijini Dar es Salaam na wa Wizara ya Viwanda na Biashara watakutana mara kwa mara kuandaa mipango ya majadiliano, kutekeleza maamuzi, kushirikiana kupanga hatua zinazofuata, kubaini na kushughulikia masuala mbalimbali yanayokabili kampuni na kuwa wataalamu wa kiufundi ili kuzishauri serikali hizo mbili. Majadiliano ya awali yatalenga katika uchumi wa kidijitali unaokua wa Tanzania, kuongeza uwezo wa kuyafikia masoko ya Marekani na Tanzania, mageuzi katika kanuni na mazingira ya kibiashara, kuandaa ziara za kibiashara kwenda Marekani na Tanzania, na kuandaa maonyesho ya kibiashara katika nchi hizo mbili. Kwa pamoja, kukuza maelewano, kujenga mahusiano mapya ya kibiashara na kujifunza na kuchangia mbinu bora za utendaji katika kufanya kazi na masoko ya Marekani na Tanzania.



Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Michael A. Battle Sr.

Baada ya muda, majadiliano ya kibiashara kati ya Marekani na Tanzania yatakuwa msingi kwa ujenzi wa uhusiano rasmi wa kibiashara ulio imara na wa kudumu utakaowanufaisha wafanyabiashara wa Marekani na Tanzania pamoja na raia wa kawaida wa nchi hizo. Iwe kwa kupeleka bidhaa bora za Kitanzania kwenye masoko ya Marekani au kwa kupanua ushiriki wa kiuchumi wa Marekani nchini Tanzania, kutengeneza nafasi za ajira zinazolipa vyema na kujenga tabaka la kati la Tanzania, makubaliano haya ni hatua ya kwanza. Majadiliano endelevu kati ya serikali zetu na sekta zetu binafsi yatakuwa muhimu sana katika kuboresha mazingira ya kufanya biashara, kuondoa vikwazo kwa biashara, kuunganisha chumi zetu, kutanzua masuala yanayokabili mnyororo wa ugavi na kufikia malengo yetu ya pamoja ya ustawi.

Majadiliano ya kibiashara kati ya Marekani na Tanzania yatakuwa jukwaa la kufanya yote hayo na kuchambua kwa pamoja na kuimarisha sera za udhibiti zitakazowavutia wafanya biashara wa Kimarekani kuja Tanzania na wale wa Kitanzania Kwenda Marekani. Wazalishaji, wenye viwanda, wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo na wa kati wa Kitanzania wana nafasi kubwa zaidi ya kunufaika kutokana na majadiliano haya. Makubaliano hayo yatajenga mahusiano baina ya nchi zetu mbili yaliyo imara, endelevu na yenye manufaa kwa pande zote.

Majadiliano ya kibiashara kati ya Marekani na Tanzania ni hatua muhimu katika kufungua uwezo na fursa kubwa ya kiuchumi iliyopo katika ushirikiano rasmi kati ya Marekani na Tanzania. Serikali peke yake haiwezi kupanua fursa kwa raia wake kwa ukubwa sawa na ambavyo inaweza kuwa kwa kuishirikisha sekta binafsi. Tanzania ni nguvu ya kiuchumi na kinara katika Afrika Mashariki na bara zima. Marekani ni mbia aliyedhamiria kwa dhati kufikia matamanio yetu ya pamoja ya maendeleo ya kiuchumi na kwa pamoja tutaleta maendeleo makubwa yasiyo na mipaka. Ni matarajio yangu kushiriki katika mkutano wa kwanza wa Majadiliano ya Kibiashara kati ya Marekani na Tanzania na kuwakaribisha wabia wapya wa kibiashara wa Marekani katika soko hili zuri.

## Shule Bombambili yaomba kuchimbiwa kisima cha maji

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

SERIKALI kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Songea pamoja na wadau imeombwa kumaliza tatizo la maji linalowakabili wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Bombambili kwa kuwachimbia kisima cha maji.

Ombi hilo limetolewa jana na Mkuu wa shule hiyo, Emmanuel Komba, wakati akisoma hotuba kwa mgeni rasmi, Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Michael Mbano, ambaye aliwakilishwa na Naibu Meya wa halmashauri hiyo, Jeremia Jerembe, wakati wa mahafali ya 14 yaliyofanyika kwenye viwanja vya shule hiyo.

Komba alisema shule hiyo pamoja na kuwapo mtandao wa bomba, lakini kuna tatizo la upatikanaji wa maji na ameiomba serikali pamoja na wadau wengine kuisaidia kupata kisima.

Shule hiyo ina zaidi ya wanafunzi 1,200 wa kidato cha kwanza hadi cha nne.

Alilitaja tatizo lingine kuwa shule hiyo haina uzio na kwa kushirikiana na wazazi pamoja na walezi wa wanafunzi wanaosoma shuleni hapo jihada zinafanyika kujenga uzio kudhibiti utoro kwa wanafunzi licha ya baadhi ya wazazi na walezi kutotimiza makubaliano ya vikao kama uchangiaji wa michango mbalimbali ikiwamo chakula kwa wanafunzi na ujenzi wa uzio.

Meya wa Manispaa ya Songea ambaye aliwakilishwa na Naibu Meya Jerembi ambaye ni diwani wa Kata ya Bombambili, alisema serikali inaendelea kufanya kazi kwa kuhakikisha miundombinu ya vyumba vya madarasa, vyumba vya maabara pamoja na ukarabati wa sakafu kwenye baadhi ya vyumba vya shule hiyo unafanyika ili wanafunzi waweze kusoma kwa uhakika.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari ya Bombambili, Dorah Kapinga, aliwaasa wanafunzi wanao hitimu elimu ya kidato cha nne kuona umuhimu wa kuzingatia wanayofundishwa shuleni na anatarajia kuona matokeo mazuri ya mitihani yao inayotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Mmoja wa wanafunzi, Azarati Rwegasira, alisema anaamini elimu waliyoipata itawasaidia zaidi kuendelea kusoma elimu ya juu zaidi na ameongeza kuwa anajisikia vizuri yeye pamoja na wahitimu wenzake kwa kuwa elimu waliyoipata inatoa fursa wao kuendelea na masomo.



## Baraza la Habari nchi za Afrika Mashariki lazinduliwa

Na Daniel Sabuni, ARUSHA

Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), zimezindua baraza la habari la nchi hizo ili kulinda maslahi ya waandishi wa habari pamoja na kuimarisha umoja wao.

Akizungumza baada ya kuzinduliwa kwa baraza hilo, Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo) na Msemaji wa serikali, Mobare Matinyi, alisema wamelipokea baraza hilo kwa mikono miwili kwa kuwa linaendana na sheria ya huduma za vyombo vya habari nchini na kwamba limekuja wakati muafaka.

"Ukisoma katika sheria ile ibara ya 24 imeeleza kuwa litaanzishwa baraza kuu la habari ambalo ni huru kwa lengo la kufanya vyombo vya habari kujidhibiti na kujipima wenyewe hivyo uwapo wa baraza hili utasaidia taaluma ya habari kufanya kazi kwa weledi," alisema Matinyi.

Katibu wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, alisema kuzinduliwa kwa baraza hilo ni ndoto ambayo imekuwa kweli kutokana na mchakato wake kuanzia mjini Kisumu nchini Kenya na viongozi wa mabaraza ya habari ya nchi ya Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda walikutana na kujadili namna ya hushirikiana ili kulinda uhuru wa habari.

"Ilikuwa ni tarehe 21 Oktoba 2018 ambapo walikubaliana wasajili baraza hilo na wanachama wake wawe kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki na hatimaye ndoto hii imekuwa kweli," alifafanua Mukajanga.

Baadhi ya waandishi wa habari kutoka nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki, akiwamo Judy Kaberya kutoka nchini Kenya, alisema watawala hawapaswi kuona vyombo vya habari kama maadui bali kushirikiana navyo lengo likiwa ni moja la kuleta maendeleo.

Barwani Mahuza kutoka Tanzania alisema licha ya ushirikiano huo kutatua matatizo yanayowakabili waandishi, utasaidia kufungua milango ya kufanya kazi nchi zingine kwani tayari tumeshakuwa kitu kimoja.

Baraza hilo lililozinduliwa na Irine Kisaka kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Jumuia ya Afrika Mashariki, Peter Mathuki.

Baraza Hilo limeweka makao yake ya makuu ya muda nchini Kenya na linaalika nchi zingine za Afrika Mashariki kuungana pamoja ili kusukuma gurudumu la habari.

Jumuiya ya Afrika Mashariki ina nchi wanachama sita akiwamo mwenyeji Tanzania, Kenya, Rwanda, Burundi, Uganda, Sudani Kusini, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo huku Somalia ikiwa kwenye majadiliano ya kutaka kujiunga.

# Serikali yasambaza Mashine X-ray hospitali za mikoa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SERIKALI kupitia Wizara ya Afya imenunua mitambo ya mionzi zaidi ya 300 (X-Ray Mashine) na kuigawa katika hospitali za mikoa nchini.

Kadhalika serikali imenunua Radiolojia (CT Scan) zaidi ya 30 na kuzigawa katika hospitali za mikoa na wilaya ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Hayo yalisemwa jana jijini hapa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk.Grace Magembe, wakati akizindua karakana ya kutengeneza na kuhifadhi vifaa tiba katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru.

Dk. Magembe alisema utekelezaji wa mradi ni ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na wadau kutoka Serikali ya Uswizi, kupitia mradi wa HPSS Tuimarishe Afya, unaotekelezwa na Taasisi ya Swiss Tropical and Public Health (Swiss TPH).

Alisema shughuli za ufundi na utaalamu zilifanywa na wahandisi wa wizara na wadau hao walichangia rasilimali fedha na vifaa tiba na vitu vingine.

"Kwa kipindi hiki serikali imeongeza kasi ya kununua vifaa tiba ikiwamo CT Scan zaidi ya 30 zimenunuliwa ambazo zimesambazwa katika hospitali zote za mikoa na X-ray mashine zaidi ya 300 na ujenzi wa majengo ya dharura 80," alisema.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Dk. Omary Chande, alisema wameweka mpango mkakati kuhakikisha shughuli zote za kitabibu zinaendelea katika hospitali hiyo.


"Tutahakikisha shughuli zinafanyika na kutunza jengo hili na vifaa vyake kwa kuwa ni jambo la msingi kwa kuwa sisi kama viongozi tutafanya ufuatiliaji wa karibu kuangalia kama huduma zinakwenda vizuri," alisema Dk. Chande.

Mwakilishi wa Ubalozi wa Uswizi nchini Tanzania, ambaye ni Ofisa Programu wa mradi, Jacqueline Matoro, alisema hadi sasa wamefanya ukarabati wa karakana mbili ambazo ziko mikoa ya Arusha na Iringa.

Alisema mradi huo umegharimu jumla ya Sh. milioni 87.1 na fedha hizo zimetumika kufanya ukarabati na kununua vifaa tiba vya karakana hiyo.

Ally Kebby, Meneja Mradi HPSS, alisema Tanzania sasa itajivunia kuwa na karakana mbili mpya za matengenezo ya vifaa tiba zilizoko mikoa ya Arusha na Iringa na itasaidia kutatua changamoto za teknolojia ya usimamizi wa afya ambazo ziliathiri utoaji wa huduma za afya.

Kwa mujibu wa Kebby, kabla ya kuanzishwa kwa mradi mwaka 2011 Tanzania ilikuwa inakabiliwa na masuala mengi yanayohusiana na usimamizi wa teknilojia ya afya ikiwamo ya miundombinu isiyofaa ya usimamizi wa vifaa, pamoja na ukosefu wa mipango madhubuti.



Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari ya Muheza Muslim, Mussa Abdi (wa tatu kulia), akikabidhi cheti kwa mmoja wa wahitimu wakati wa mahafali ya 23 ya kidato cha nne ya shule hiyo, wilayani Muheza mkoani Tanga mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mkuu wa shule hiyo, Ramadhani Makea (kushoto), Meneja wa shule hiyo, Mohamed Kijunge (wa pili kushoto) na (wa pili kulia) ni Mkurugenzi wa shule hiyo, Twaha Msenga. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Tz yapongezwa utoaji huduma malipo yasiyotumia fedha taslimu

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

TANZANIA imepongezwa kwa kupiga hatua chanya ya kuunganisha mifumo ya utoaji huduma ya malipo yasiyotumia fedha taslimu na uundaji wa miundo ya jumla ya serikali, katika ngazi zote za serikali na kudhibiti mapato.

Vilevile, amepongeza asasi za kiraia kwa kutoa michango muhimu katika kuongeza uelewa wa wananchi, masuala ya maendeleo, kutetea rushwa au kupinga ukatili wa kijinsia na kueleza serikali changamoto wanazokumbana nazo kuleta haki na usawa.

Pongezi hizo zimetolewa jana jijini Arusha na Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot, wakati wa ufunguzi wa wiki ya Azaki, inayokutanisha mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) kutoka ndani na nje ya nchi.

Chassot alisema ukusanyaji wa fedha kwa kutumia mfumo huo, unaotekelezwa na serikali umewezesha kuunganisha uundaji wa miundo ya jumla ya serikali, katika ngazi zote za serikali na kufanikiwa kukusanya mapato makubwa na teknolojia kukua.

"Kama tunataka twende mbele kidijitali, lazima sasa Azaki twende na mifumo hii ambayo itaongeza ufanisi na uwazi, katika upatikanaji wa taarifa za NGOs, ambazo zikitumiwa vizuri italeta manufaa zaidi," alisema.

Aliwaomba washiriki kuzingatia majadiliano yanayofanyika ili yakasaidie kutoa suluhu ya changamoto za wananchi kwa kuhakikisha makundi yote ya jamii yananufaika, kutokana na maendeleo ya teknolojia na kuangalia hakuna anayeachwa nyuma.

Meneja Mahusiano wa Benki ya Stanbic, Doreen Dominic, alisema benki hiyo inashikilia nafasi ya nne kwa ukubwa nchini, kutokana na kuboresha huduma kidijitali na kuboresha maisha ya Watanzania, hususan vijana na wanawake katika kuwapatia maendeleo.

"Benki katika kuendana na masuala ya kijamii tunatoa mada juu ya kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha, kwa kutumia teknolojia ikiwemo dijitali kuonyesha utofauti wa kiuchumi na kuwezesha watu ambao bado hawajafikiwa," alisema.

Mrajisi wa Asasi za Kiraia kutoka Zanzibar, Ahmed Khalid Abdulla, alizitaka asasi za kiraia kusaidia jamii katika kufikisha taarifa za matumizi sahihi ya kidijitali ili waweze kutumia kama fursa zilizopo kujikwamua kiuchumi na maendeleo endelevu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Foundation for Civil Society, Francis Kiwanga, alitoa rai kwa Watanzania hususan vijana kutumia teknolojia kwa matokeo chanya, ili wapate fursa mbalimbali za kujikwamua kiuchumi, ikiwamo kujua teknolojia mpya ya akili bandia (AI).



## Wanafunzi shuleni, vyuo vikuu wanolewa kuhusu maadili

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Magharibi, imeanza kutoa mafunzo juu ya uanzishwaji wa klabu za maadili shuleni na vyuo vikuu mkoani Shinyanga.

Lengo likiwa ni kujenga msingi bora wa maadili kwa wanafunzi wakiwa shuleni.

Katibu Msaidizi Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Magharibi (Tabora, Kigoma, Shinyanga Simiyu), Gelard Mwaitebele akizungumza katika mafunzo ya walimu walezi shuleni na vyuoni, alieleza kuwa uanzishwaji wa klabu hizo utasaidia kuandaa kizazi bora chenye maadili.

Alisema, tatizo la ukosefu wa maadili lipo katika jamii ambalo huanzia ngazi za chini, hivyo wao wameona ni vyema kuanza kutoa mafunzo kwa walimu hao walezi watakaoanzisha klabu hizo za maadili na kuwaandaa wanafunzi kuwa na maadili mema wanapokua uraiani.

Ofisa Maadili Kanda ya Magharibi, Onesmo Msalangi, alizitaka klabu hizo zikasaidie kulinda maadili katika nchi, huku akisisitiza kuwe na ukaribu mkubwa kwa watoto hasa katika kipindi hiki ambacho maadili yameshuka kwa kiasi kikubwa.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga, Ibrahim Makana, akizungumza katika mafunzo hayo alisema kuwa kuanzishwa kwa klabu hizo kutalifanya taifa kwa na watu wenye maadili na uzalendo katika nchi yao na kuzalisha viongozi waadilifu.

Wanufaika wa mafunzo hayo, waliishukuru serikali kwa kuanza kutoa elimu hiyo na kuahidi kutekeleza maagizo ya kuanzisha klabu hizo za maadili shuleni na kwenye vyuo ili kuandaa kizazi chenye maadili mema.

**Ofisa Maadili Kanda ya Magharibi, Onesmo Msalangi, alizitaka klabu hizo zikasaidie kulinda maadili katika nchi, huku akisisitiza kuwe na ukaribu mkubwa kwa watoto hasa katika kipindi hiki ambacho maadili yameshuka kwa kiasi kikubwa.**

# Simulizi ya wanufaika TASAF walivyouaga umaskini

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WANUFAIKA wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) mkoani Shinyanaga wameeleza namna mfuko huo ulivyowasaidia katika kuinua kimaisha ikiwamo kusoma hadi elimu ya juu.

Walibainisha hayo kwa nyakati tofauti walipotembelewa na Nipashe katika maeneo yao kujua mchango wa mfuko huo katika jamii.

Walisema kuwa mfuko huo umekuwa ukiziinua kaya maskini hususani kwa wanafunzi ambao wa wanasomeshwa kwa ruzuku hadi vyuo vikuu.

Mkazi wa Kijiji cha Ishinabulandi Kata ya Samuye Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Grace Mahona (23) alieleza kuwa mfuko huo umemsaidia katika masomo yake kuanzia Shule ya Msingi Ishinabulandi na sasa yuko Chuo Kikuu cha Dar-es -Salaam (UDSM) mwaka wa pili akisoma Shahada ya Elimu.

Alisema licha ya familia yake kuwa na hali ngumu kiuchumi mfuko huo umemsaidia kufikia malengo yake ya kielimu kwani wenzake aliokuwa akisoma nao waliishia njiani kwa sababau mbalimbali ikiwemo utoro, kubeba ujauzito na baadhi kukimbilia mjini kutafuta maisha kulingana na hali za familia zao.

Aidha, alisema mama yake alisajiliwa kwa mara ya kwanza kupokea ruzuku hiyo mwaka 2015 akipokea Sh. 72,000 fedha ambayo iligawanywa kwa kununua mahitaji yake ya shule, taulo za kike, chakula cha familia na kiasi kikaelekezwa kwenye biashara ya ujasiriamali wa kuuza mboga.

"Niwe mkweli kwa ugumu tuliokuwa nao kwenye familia yetu ilikuwa kidogo nikate tamaa ya kusoma, kwani nilikuwa nakwenda shule bila kula na wenzangu niliosoma nao wengi wameishia njiani kutokana na uchumi kuyumba," alisema Grace.

Ndalo Luhende (56) mmoja wa wanufaika hao alisema ugumu wa maisha ulifika kwenye familia yake baada ya mumewe kufariki, hivyo kuamua kujiunga katika mfuko huo.

Alisema katika ruzuku yake alihifadhi kiasi na kunzisha biashara ya kuuza viti vya kukalia, ambapo ananunua kimoja kwa Sh. 2500 katika Kata ya Tinde na kuja kuuza kimoja kwa Sh.5,000 hadi Sh. 7,000.

Mkazi mwingine wa Kijiji cha Wame Kata ya Kilago Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Mrisho Bundala (46) aliomba kuondolewa kwenye upokeaji wa ruzuku ya (TASAF) baada ya kufanikiwa kumiliki makazi pamoja na kuwa na mashamba ya kumpatia chakula cha kutosha msimu mzima kila mwaka.

Alisema alisajiliwa na kupokea ruzuku yake kwa mara ya kwanza mwaka 2015 kwa kupokea Sh. 48,000.

Aidha, Bundala alisema mara ya mwisho kupokea ruzuku yake ilikuwa Novemba na Desemba mwaka jana na mwaka ambapo alifika katika Ofisa za TASAF Wilaya ya Kahama na kuomba kuondolewa kwenye mpango ili watu wengine wapewe nafasi kwasababu yeye anauhakika wa kupata chakula tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

Mke wa mnufaika huyo, Maria Charles (37) alisema yeye ndiyo aliyemshawishi mumewe kujiondoa katika upokeaji wa ruzuku na kuwapatia nafasi hiyo watu wengine wenye maisha magumu kama waliyokuwa nayo wao awali, kwasababu wao wanauhakika wa kupata chakula cha kuendesha maisha yao.



Sehemu ya wanachama 250 wa Jukwaa la Wanawake wa Saccos Taifa kutoka mikoa yote nchini, wakishiriki mkutano wa kujadili masuala mbalimbali yanayohusu ushirika, akiba, mikopo, elimu, kuimarisha mahusiano pamoja na kubadilishana uzoefu ili kujiimarisha kiuchumi na kupata fursa mbalimbali, jijini Mwanza jana. **PICHA: ROSE JACOB**

# Akutwa amefariki nyumbani, mwili wakutwa na jeraha

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MZEE Elias Mulanda (80) mkazi wa Kijiji cha Ilunda mkoani Mwanza amekutwa amefariki, huku mwili wake ukiwa umechomwa na kitu chenye ncha kali katika maeneo ya shingoni.

Akielezea tukio hilo Mwenyekiti wa Kijiji cha Ilunda, Theleza Mbizangula alisema kuwa tukio hilo lilitokea majira ya saa nne asubuhi ambapo alipokea simu kutoka kwa ndugu wa marehemu kumjulisha juu ya tukio hilo.

Alisema kuwa baada ya kufika nyumbani kwa mzee huyo watoto na baadhi ya ndugu wa marehemu walimuonesha mwili, ndipo alipogundua kuwa mwili huo una majeraha sehemu za shingo.

Aliendelea kusema kuwa baada ya kuangalia kwa makini waligundua kuwa mwili huo ulikuwa umekatwa shingo kwa kitu chenye ncha, hivyo kusitisha suala la kumuosha na kutoa taarifa katika mamlaka husika.

Mwenyekiti huyo aliwataka wananchi wanapokuwa na migogoro wafike kwa viongozi ama wakae kama ndugu ili kupata suluhu na siyo kujichukulia sheria mkononi.

Mtendaji wa Kijiji cha Ilunda, Furaha Bahati alisema kuwa suala hilo wanaliachia Jeshi la Polisi kwa ajili ya kuendelea na uchunguzi wao ili kubaini chanzo cha tukio hilo na wahusika wake ili taratibu nyingine za kisheria ziendelee kuchukua mkondo wake.

Wakizungumzia tukio hilo watoto wa marehemu Sikujua Mulanda na Sagija Mulanda walisema tukio hilo limewasikitisha kwani wao waliendа kumsalimia baba yao majira ya asubuhi akiwa mzima na wakaelekea shambani na baada ya muda mfupi wakaambiwa baba yao amefariki.

Jeshi la polisi wilayani Sengerema lilifika eneo la tukio na kuuchukua mwili wa marehemu, kisha kuupeleka katika Hospital ya Wilaya ya Sengerema kwa ajili ya uchunguzi.



Ukurasa 12

**Viongozi mjipime na darasa siasa safi mliyopewa na Biteko**



Ukurasa 13

Miriam nyota inayotembea na utetezi 50/50 kila kona



Ukurasa 14

**RAIS MAHMOUD ABBAS**

**Mwenye uvumilivu anayeonyesha jinsi ya kufikia amani**


# siasa

JUMATANO OKTOBA 25, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


UTEUZI WA MAKONDA

# Wadau waguna ni mwenezi aliyepigwa 'X' Marekani

• Wabashiri atatumika kuvuna ushindi uchaguzi 2024, 25

**Na Sabato Kasika**

JULAI 2020 Paul Makonda, ni Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam, akiwa na wadhifa mwingine begani wa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, anaoutumia kwenye kampeni mbalimbali.

Ni kijana ambaye wana Dar es Salaam, wanakumbuka jinsi alivyowagusa, lakini wana jimbo la Kigamboni wanayo namna nyingine ya kumzungumzia.

Watasema alikuwa mmoja wa watiania wa ubunge katika jimbo lao, na wakati huo kukiwa na minong'ono kuwa anaandaliwa kuwa na majukumu mazito serikalini, lakini bahati haikuwa yake, alishindwa kura za maoni hazikutosha na tangu wakati huo yuko nje ya shughuli za umma na za kisiasa, takribani miaka minne sasa.

Leo anaongea lugha nyingine baada ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kumteua kuwa Katibu wa Halmashauri Kuu (NEC) Itikadi na Uenezi akichukua nafasi ya Sophia Mjema anayekuwa Mshauri wa Rais Masuala ya Wanawake na Makundi Maalum.

Uteuzi huo wa Makonda umezusha mjadala katika mitandao ya kijamii, kukiwa na makundi yanayompongeza kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo, jingine 'likiguna' likimaanisha lina ya moyoni.

Wachambuzi na wadau wa masuala ya siasa wanaozungumza na Nipashe kuhusu uteuzi wa wadhifa mpya wa mkuu wa zamani wa mkoa wa Dar es Salaam, wanasema wanasubiri kuona kama amebadilika.

Ananilea Nkya ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), anaeleza kushangazwa na yaliyotokea, akisema kuna haja ya kumpa muda ili



Paul Makonda, Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM, Itikadi na Uenezi. **PICHA: MTANDAO**

kuona kama amekaa nje ya mfumo wa uongozi na kubadilika.

"Yapo mengi ambayo alituhumiwa nayo akiwa kwenye uongozi, lakini pia amekaa nje kwa muda mrefu, huenda amejifunza na anaweza kuwa amebadilika, hivyo tusubiri tuone," anasema Ananilea.

Anafafanua kuwa mtu anapokuwa nje ya mfumo na kuishi na wananchi au raia wa kawaida, wapo wanaojifunza kuheshimu wengine na kuwa sehemu ya jamii na kwamba huenda Makonda naye amejifunza.

"Ndani ya mfumo alikuwa mbabe asiyejali wala kuheshimu sheria, lakini ninadhani kuwa kwake nje anaweza asiwe yule Makonda ambaye alifanya kila analotaka bila kizuizi," anakumbusha.

### NGUVU YA 2025

Kada wa CCM Thomas Ngawaiya anasema, ujio wa Makonda katika nafasi hiyo ni turufu au nguvu ya kuipa ushindi CCM katika uchaguzi wa 2025, kwa maelezo kwamba ni mbunifu mwenye mbinu nyingi za kupata ushindi.

Mbali na ubunifu, anasema Makonda si mwoga ana uwezo wa kupenya pale wengine wanaposhindwa na kwamba amerejeshwa wakati muafaka ili kukisaidia chama kupata ushindi kwenye chaguzi za 2024 wa serikali za mitaa na mkuu wa 2025.

"Mama hajakosea kumteua anajua mbinu za Makonda na hata ubunifu wake katika siasa. Hayo mambo mengine ambayo amelaumiwa, ukweli ni kwamba hakuna binadamu aliyekamilika," anamtetea Ngawaiya.

Anasema chama kinataka watu wa aina yake, ambao ni wepesi kutumwa na kutekeleza jambo bila woga, kwa maelezo kwamba siasa zinahitaji mbinu nyingi ili kupata ushindi.

### KUINGIWA HOFU

Mchambuzi wa siasa, Hebron Mwakagenda anasema nje ya chama Watanzania wanamchukulia Makonda kama mtu pengine asiyefaa kuwa kiongozi, ndani kuna sintofahamu kati yake na vigogo wenzake na kwamba kuna woga pia juu yake nje na ndani ya chama.

Mwakagenda anasema uteuzi wake unaleta mkanganyiko na hofu kutokana na jinsi alivyoonekana kuwa kama mtu wa pili katika nchi baada ya Rais akawa haogopi wala kuheshimu watu wazima kwa wakubwa hata viongozi wenzake.

"Nimesoma pongezi za Nape na Chongolo kwake, lakini ninazichukulia kama hofu, huenda wanahofia kwamba anaweza kuwa nguvu kubwa kama alivyokuwa wakati akiwa mkuu wa mkoa ," anasema Mwakagenda.

Aidha, pamoja na hayo, baadhi ya vigogo wa CCM huwa hawaivi na Makonda, hali ambayo mchambuzi huyo anafafanua kuwa pengine katika utendaji kazi wake huenda usiwe na ufanisi kutokana na tofauti hizo.

"Kwa hiyo sisi wengine yetu macho na masikio kushuhudia jinsi ambavyo atafanya kazi yake hiyo mpya chini ya baadhi ya viongozi ambao alikuwa haivi nao wakati wa awamu ya tano," anasema Mwakagenda.

### UTUNDU/ UBUNIFU

Mwanasiasa James Mbatia anasema Makonda ni mtundu na mbunifu tangu mdogo, na kwamba akiendeleza kipaji hicho kinaweza kumsaidia kuongoza chama na kusaidia nchi kwa ujumla.

"Nafasi aliyopewa ni kubwa, atumie hekima na busara, aachane na utoto, watu wanataka kuona hekima na busara zake, kwani kwa sasa amekuwa mtu mzima aachane na tabia za kitoto," anasema Mbatia.

Mwanasiasa huyo anaongeza kuwa nafasi yake katika chama ambacho kinaongoza nchi ni kubwa, na kwamba hapaswi kujadili watu bali masuala yanayohusu maendeleo ya taifa.

"Akiweza kufanya hivyo, atakuwa kiongozi mzuri, hasa kutokana na ukweli kwamba ana uwezo wa kushawishi, ila anapungukiwa na hakima na busara, ambavyo ni vya muhimu kwa binadamu," anasema.

INAENDELEA UK. 14

# Viongozi mjipime na darasa siasa safi mliyopewa na Biteko



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ,Dk. Dotto Biteko, (kushoto),alipokutana na Rais mstaafu Jakaya Kikwete, jimboni Chalinze hivi karibuni. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Reubeni Lumbagala,**

DODOMA

BABA wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, anakumbukwa kwa haya aliyosema kuwa ili Tanzania iendelee inahitaji vitu vinne;watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Uwepo wa vitu hivyo vyote vinne na mfumo madhubuti wa kuratibu utendaji kazi, utoaji haki, umahari na nidhamu ni dhahiri maendeleo ya kweli yanayogusa maisha ya watu yataweza kufikiwa kwa taifa kuwa na mafanikio makubwa.

Hivi karibuni kuna jambo moja kati ya manne yaliyoainishwa na Baba wa Taifa ambalo ni siasa safi nayo ndiyo maisha kwa vile inagusa kila eneo la mwanadamu kuanzia elimu, chakula, tiba, ibada na hata kiinua mgongo au mafao uzeeni, linaibuliwa.

Hakuna namna ambayo ustawi na maendeleo ya watu yanaweza kujadiliwa na kufikiwa bila uwepo wa siasa lakini iwe siasa safi yenye tija kwa mwananchi inayohakikisha kuwa hakuna anayeachwa nyuma.

Kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya wanasiasa maeneo mbalimbali kushindwa kufanya siasa safi zenye kugusa maisha ya Watanzania maskini badala yake kujikita kutoa lugha za kebehi, dharau na zisizo na staha. Siasa safi ndizo zenye kujenga hoja, tena zinazojikita kujibu mahitaji ya wananchi, kuwapa matumaini badala ya kuwakatisha tamaa na kuwakejeli.

Mapema mwezi huu akiwa mgeni rasmi wa mkutano wa wanachama na viongozi wa CCM uliopokea taarifa ya utekelezaji wa ilani ya chama hicho Chalinze unaoandaliwa na mbunge wa jimbo hilo Ridhiwani Kikwete, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, anawapa darasa la siasa safi wanaCCM na Watanzania.

> “Kufanikiwa kwa haya yote yanategemea utendaji kazi wa viongozi wenye dhamira ya dhati ya kubadili maisha ya watu wanaowaongoza na kuwatumikia siyo kuwa kiongozi ili unufaike na wale unaowapenda.



Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, mwasisi wa falsafa ya mambo manne yanayohitajika ili kupata maendeleo.

Kwanza anasisitiza kwamba ili kuwa na maendeleo ni vema kufanya kazi za kubadili maisha ya watu badala ya siasa za maneno, akiwataka kwanza kushikamana, kuthaminiana, kuvumiliana na kuangalia yanayowakera pamoja badala ya yale yanayowatenganisha .

Anawaambia wasiingie kwenye matusi na kejeli na kazi yao iwe ya kuyasemea yale yaliyofanywa na serikali kwa vile wananchi wanachohitaji ni huduma wawapelekee maendeleo huko waliko, fedha zilizopo zitumike kwa kiwango kinachotakiwa watu waone maisha yao yakibadilika, ndilo analosisitiza Dk. Biteko.

Hilo ni darasa, ni shule kwa viongozi kwa sababu anafahamu kiu kubwa waliyonayo wananchi ni utatuzi kero zao na kugusa maisha yao kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo. Utatuzi wa kero za wananchi, unategemea utendajikazi madhubuti wa viongozi waliopewa jukumu na ridhaa ya kuwatumikia Watanzania ndiyo viongozi wa kuchaguliwa, wa kuteuliwa na watumishi wa umma wanaowajibika moja kwa moja kuwatumikia wananchi katika maeneo yao ya kazi.

Kwahiyo, viongozi wanawajibika moja kwa moja kufanya siasa za kubadili maisha ya watu ili kuchochea maendeleo katika jamii na nchi kwa ujumla siyo kuwa na umimi, kujiangalia wenywe' na wakati mwingine kupuuza watu.

Dokta Biteko anataka kasi ya kuboresha huduma za kijamii kwa wananchi kwani hiyo ndiyo siasa safi yenye kubadili maisha ya watu. Wananchi wanataka kupata elimu, afya, maji, umeme, barabara na miundombiny bora.

Pia wanahitaji kuboreshewa shughuli zao, mathalani, kupata pembejeo kwa ajili ya kilimo, mifugo na uvuvi yote hayo yaambatane na uwepo wa masoko ya kuuza bidhaa zao. Lakini pia wanayo kiu ya kuboreshewa miundombinu ya barabara na ujenzi wa masoko ili waweze kufanya biashara zao katika mazingira mazuri ili hatimaye waweze kupata kipato kwa ajili ya familia zao na kuchangia maendeleo ya nchi yao.

Kufanikiwa kwa haya yote yanategemea utendaji kazi wa viongozi wenye dhamira ya dhati ya kubadili maisha ya watu wanaowaongoza na kuwatumikia siyo kuwa kiongozi ili unufaike na wale unaowapenda.

Aidha, Dk. Biteko anatoa rai kuzingatia matumizi bora na ya kiuaminifu ya fedha za umma zinazotengwa na serikali katika kughramia miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo ndiyo inayobadili maisha ya Watanzania popote walipo.

Hii ni kutokana na ukweli kuwa kubadili maisha ya watu kunakwenda sambamba na utekelezaji wa mipango na shughuli za maendeleo yao ambapo bila nidhamu ya kutumia fedha hizo, miradi hiyo itakwama na hivyo maisha ya wananchi yataendelea kuwa duni.

Hivyo basi, mkazo wa Dk. Biteko wa kutaka fedha za miradi zitumike kwa kiwango kinachotakiwa ni namna bora ya kufanikisha mkakati wa serikali wa kubadili maisha ya wananchi wake kutoka maisha ya chini hadi maisha bora.

Kimsingi, kwa wanasiasa kutaka kuungwa mkono na wananchi bila kuwa na mikakati thabiti inayopimika ya kubadili maisha ya Mtanzania ni kupoteza muda tu. Wananchi wa sasa wanajua aina ya kiongozi wanayemtaka ili washirikiane nae katika juhudi za kujiletea maendeleo, kiongozi huyo ni yule anayefanya siasa zenye mrengo wa kuboresha hali za wananchi wake. Ushirikiano na mshikamano vilevile ni moja ya msingi muhimu wa kufanya siasa safi.

Viongozi ni lazima washirikiane kikamilifu na wananchi wao ili kuunganisha nguvu ya pamoja na hatimaye kufikia maendeleo ya kweli. Pengine, ni muda muafaka sasa kwa wanasiasa kubadili aina ya siasa. Wakati na mazingira ya siasa nchini yamebadilika. Ni lazima kujikita katika siasa safi, bila kufanya hivyo, wanasiasa wataangukia pua, kama hawaamini wajaribu waone.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Mlali Sekondari ya mkoani Dodoma.***

***Maoni: 0620 800 462.***

Na Christina Mwakangale

NYOTA njema huonekana alfajiri na dalili ya mvua ni mawingu. Ndivyo unavyoweza kumtafsiri Miriam Mkanza, ambaye tangu akiwa shule ya msingi amekuwa kiongozi na sasa ni mwanachuo Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), akiwa na nyadhifa kadhaa.

Mwanafunzi huyo mwenye miaka 22 , amepata elimu ya msingi katika Shule ya Tumbi iliyoko Kibaha mkoani Pwani, kwa haiba unapomtazama na namna anavyojieleza utapata tafsiri nyingi, mojawapo ni ujasiri uliomo ndani yake.

Pia, anaendana na kile anachokishuhudia mbele ya mabinti waliokusanyika kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, jijini Dar es Salaam, akionyesha kuwa ana talanta au kipaji cha uongozi.

Miriam pamoja na wenzake wanaposherehekea siku yao, anasema alianza kuwa jasiri mapema akiihudumia jamii ndani ya shule za msingi na sekondari na chuoni kwa kuwa sehemu ya viongozi, hasa kusimamia ajenda ya mwanamke; usawa wa kijinsia na hatua za kuzifikia uwiano wa 50/50 uongozini.

Anapozungumza na Nipashe, anasema kila anapopewa nafasi ya kuwasilisha mada mbele ya mabinti, anajikita kuwajengea uwezo ili kuwa viongozi wa sasa pale walipo kwa maana ya shuleni ama vyuoni, kwa kuelezea maisha yake na kusimulia hali halisi ya maisha aliyopitia.

"Nilichaguliwa kujiunga na Shule ya Ufundi Moshi mwaka 2014. Ilikuwa kawaida shuleni hapo wasichana kusoma masomo ya sanaa na sio sayansi. Ila mimi nikachagua kusomea umeme na katika darasa zima wasichana tuliokuwa kwenye tahsusi hiyo tulikuwa wawili, darasa lote likijaa wavulana."

"Ikafika muda wa kutafuta kiongozi, nimo na hata ikiwa tulikwenda kuvaa overoli nilikuwa mstari wa mbele, ujasiri wangu uliwapa moyo wasichana wengine waliofuata nyuma yangu shuleni," anasema Miriam.

Hakupitwa na uongozi, Moshi Tech, akisema alikuwa kiongozi wa bweni na wakati wa kuuwani alijifanyia kampeni kikamilifu na moja ya kitu kilichombeba ni kuaminika na wenzake kwa kuwa alikuwa ni miongoni mwa wasichana wachache waliomudu masomo ya sayansi akivunja mwiko kuwa wanaoyaweza ni wavulana pekee.

"Walinitazama wakisema huyu anayegombea anasoma sayansi atashindwaje kutuongoza? Kwa hiyo nilikubalika na mabweni hayakuwa mbali ...." Anasema.

Miriam anaongeza kuwa masomo ya sayansi yanaongeza kujiamini na ilikuwa akigombea wanajua kuwa ataweza, halafu ukiwa kiongozi inabidi ufanye vizuri.

Aidha, darasani ujitahidi uwaongoze kimasomo kadhalika kwenye majukumu ya kuchaguliwa, siyo wenzio wakuzidi kimasomo hilo lazima likufanye kuwa jasiri.

Anafafanua kuwa nafasi za uongozi alizoshika akiwa shule ya msingi ni kuwa mmoja wa wasimamizi akiwasilisha wanafunzi kwenye chumba cha mtihani wa darasa la saba, kuhakikisha kuwa mambo yanakwenda kama ilivyopangwa mfano, mitihani kuwa salama, kuna ulinzi na ratiba hufuatwa.

Akiwa sekondari ni uongozi wa bweni na Katibu wa Klabu ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

"Ili kufikia 50/50 ni lazima wanafunzi wa kike tusome sayansi ili kwenye uhandisi tuwemo. Nimesoma uhandisi wa umeme sekondari. Nikajiunga chuoni DIT, diploma kusomea Sayansi ya Chakula na Ufundi na nimebaini hata huko tunakotoka hasa vijijini wanakuangalia wewe, ili uwashawishi huko nako nikaambiwa niwe kiongozi wa darasa".

Miriam anasema akiwa DIT ngazi ya diploma ameshika nyadhifa tofauti chuoni, ikiwamo kuwa mbunge, naibu waziri wa jinsia na maafa na mjumbe wa UVCCM DIT.

"Lazima ujiamini kama unataka kufanikiwa napenda kuhudumia jamii na lazima uwe na ratiba kwamba muda huu ni wa masomo, kupumzika, kuhudumia jamii. Wanawake na wanaume wote tumeumbwa na Mungu. Tunaweza

"Kwa nini wanawake wawe na kazi zile nyepesi tu? Yaani masomo ya sanaa na wanaume ndio wasomee sayansi? Ili tufikie 50/50 lazima tusome sayansi ili kuweka ushindani," anasema Miriam.

Anakumbusha kuwa alipomaliza diploma mwaka 2021 DIT ameendelea na masomo chuoni hapo akisoma shahada ya sayansi na teknolojia ya maabara, huku akishika nafasi tofauti uongozini chuoni.

"Nilipomaliza kozi ya kwanza nikajiunga shahada ya sayansi ya maabara na teknolojia. Ila awali niliona ni ngumu. Nashauri mitandao ya kijamii tuitumie kutimiza ndoto zetu katika kompyuta angalia vipindi vya kiteknolojia au katika televisheni, sio unaangalia filamu muda wote, tazama vipindi tofauti na vya uongozi ili uwe kiongozi,"anasema

Anaeleza kuwa akiwa mwaka wa pili chuoni anachaguliwa kuwa Naibu Spika. Pia Waziri wa Jinsia na Mahusiano, katika nafasi hiyo hakuna aliyejitokeza walikaa pembeni, kwa sababu walishaona anaweza hata kwenye masomo wakaona wamwachie akapenya kiurahisi.

Anakumbusha kuwa kila mahali unahitajik usawa katika shughuli za maendeleo ya jamii, ili kufika pamoja kila kitu kinawezekana. Kuna viongozi wa aina mbili;wa kuzaliwa na kujifunza.

Anasema anajengwa kiongozi na wadau tofauti kama vile TGNP, mama yake mzazi na kutumia muda wa ziada mitandaoni kujifunza namna gani Wanawake wengine wamefanikiwa kuwa viongozi.

Hivi sasa Miriam akiwa chuoni DIT mwaka wa tatu wa masomo, ni kiongozi wa darasa mbunge, waziri wa jinsia na mahusiano na mbaraza (mjumbe wa baraza ) wa UVCCM seneti ya Dar es Salaam.

"Changamoto katika uongozi nilizonazo sasa na kuzipitia kama waziri ni ninapopokea taarifa ya ukatili yule mtoa taarifa anaogopa suala lake kwenda mbele akihofia labda atachekwa, atatengwa. Kuna tukio moja lilitokea chuoni dada alichanwa na kisu na mpenzi wake, baadae alinifuata akasema muachie kwani bado anampenda eti wana malengo. Kwa sababu yule kaka adhabu ilikuwa ni kufukuzwa chuo."

Miriam anautaja ushirikiano upatao kwenye familia yake. : "Tupo wawili na kaka yangu na familia, ilipenda nilichokuwa nakifanya na nilionyesha nia yangu na waliniamini na nilikuwa namuomba Mungu pia."

Anaeleza kuwa wanawake wanaweza na kwamba mwanamke anaweza kufanya mambo mengi kwa wakati mmoja kuliko mwanaume. Anapika, anaelea mdogo wake, anafua nguo, hivyo wanaume wawaepushe wasichana na ukatili ambao unaweza kuwakumba mabinti, ili watoto wa kike wafanikiwe.

"Kaka yangu aliishia sekondari na yupo na maisha yake kwa sasa, ila mimi nikaamua kujitahidi kusonga mbele na masomo yangu."

Awali, akifungua warsha jumuishi kwenye maadhimisho hayo, Flora Ndaba, kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania TGNP anatoa wito kwa wasichana kupanga muda wao kwenye ratiba ya majukumu yao ya kila siku.

"Bidii, bila hofu inakujenga kijana, kila unayetaka kuwa kiongozi jionyeshe taswira yako, ili watu nje wakuone, tumia muda wako mwingi katika ndoto zako," anasema.




Miriam Mkanza akiwapa somo wanafunzi wa shule za msingi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani.
**PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Miriam nyota inayotembea na utetezi 50/50 kila kona

> Kwa nini wanawake wawe na kazi zile nyepesi tu? Yaani masomo ya sanaa na wanaume ndio wasomee sayansi? Ili tufikie 50/50 lazima tusome sayansi ili kuweka ushindani.

RAIS MAHMOUD ABBAS

# Mwenye uvumilivu anayeonyesha jinsi ya kufikia amani Jerusalem



Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken (kushoto) akiwa na Rais wa Mamlaka ya Wapalestina, Mahmoud Abbas. **PICHA: AFP**

**Na Mwandishi Wetu**

AMEKUWA Mwenyekiti wa Chama cha Ukombozi wa Palestina (PLO) tangu 2004, aidha ndiye Rais wa PNA kuanzia Januari 2005, na Rais wa Jimbo la Palestina Mei 2005. Ndiye Mahmoud Abbas, Rais wa Mamlaka ya Wapalestina, au Palestina Huru.

Mkuu wa Mamlaka ya Palestina Mahmoud Abbas , kwa muda mrefu amekuwa akitajwa kuwa ni rais wa taifa huru la Wapalestina, hata hivyo taifa huru la Kipalestina bado halijapatikana.

Abbas, hajakaa kimya katika kupata ufumbuzi wa mgogoro wa Palestina na Israel, hivi karibuni Rais wa Palestina analiambia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwamba amani ya Mashariki ya Kati haitapatikana hadi Wapalestina wapewe haki kamili.

"Wale wanaofikiri kuwa amani inaweza kuwepo katika Mashariki ya Kati bila watu wa Palestina kufurahia haki zao kamili na halali za kitaifa watakuwa wamekosea," Abbas anauambia mkutano wa kila mwaka wa Umoja wa Mataifa wa Septemba mwaka huu.

> Mafanikio makubwa zaidi katika maisha yangu ni kuwapigania ninyi watu wa Israeli na kwa ajili ya nchi yetu. Shabbat Shalom.

Kiongozi huyo mkongwe mwenye miaka 87 anatoa wito mpya kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, kuitisha mkutano wa kimataifa kuhusu kuunda taifa huru la Palestina.

Anasisitiza kuwa Mkutano wa Umoja wa Mataifa unaweza kuwa fursa ya mwisho ya kuokoa na kupata suluhisho la serikali mbili na kuzuia hali kuwa mbaya zaidi na kutishia usalama na utulivu wa eneo la Mashariki ya Kati na dunia nzima, Abbas anasema.

Hotuba ya Abbas inakuja wakati ambao Marekani inapiga hatua katika kufanikisha makubaliano kati ya Israeli na Saudi Arabia.

Marekani, kihistoria ndiyo msuluhishi wa amani kati ya pande hizo mbili, inadaiwa kuwa imekata tamaa katika mazungumzo mazito na serikali ya Israel.

Itakumbukwa kuwa kuanzia mwanzoni mwa 2020 uongozi wa Wapalestina umegawanyika, kuna wanaojipambanua na Ukanda wa Gaza unasimamiwa na kundi la Hamas ilhali mamlaka ya Palestina pamoja na kundi la huku Fatah ikishikilia udhibiti wa Mamlaka ya Kitaifa ya Palestina katika Ukingo wa Magharibi wa Mto Jordan kupitia kwa Rais Abbas ,lakini pia udhibiti wa kambi za wakimbizi wa Kipalestina.

Mamlaka ya Wapalestina yanahusu Ukanda wa Gaza na Ukingo wa Magharibi, pamoja na eneo la Jerusalem Mashariki, hata hivyo Mamlaka inasimamiwa kiasi kidogo cha sehemu ya Ukingo wa Magharibi, lakini eneo kubwa la Ukingo wa Magharibi wa Jordan bado iko chini ya udhibiti wa moja kwa moja wa Jeshi la Israel na raia wake.

Licha ya Israel kuulipua Ukanda wa Gaza, ambao kwa sasa unaongozwa na Hamas ambacho ni chama cha kisiasa chenye mrengo wa wapiganaji dhidi ya Israel , uongozi wa Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, unajitetea kuwa Hamas ndiyo, walioanzisha mashambulizi mapema mwezi huu na kutishia amani ukanda huo.

Itakumbukwa Oktoba 7 2023, makundi ya wapiganaji wa Kipalestina huko Gaza ya Hamas yalianzisha "Operesheni Mafuriko ya Al-Aqsa " dhidi ya Israeli, kujeruhi, kuua, na kukamata vikosi vingi vya Israeli na raia.

Kuanzia hapo Israel ilitangaza vita na kuanza kampeni ya mashambulizi makubwa ya mabomu huko Gaza na kusababisha majeraha na vifo vya maelfu ya Wapalestina, ambapo zaidi ya asilimia 65 ni wanawake na watoto.

Lakini lawama zinaelekezwa kwa Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, ambaye ameongeza mzozo kwa kusisitiza kuwa na makazi zaidi katika Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kwa mabavu na taifa hilo.

Katika kile kinachoonyesha kuwa Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, pengine amesababisha mashambulizi ya mwanzoni mwa Oktoba ni kile kinachoonekana kuwa hasikii la mtu.

Mwezi uliopita alipokuwa akihutubia Kikao cha 78 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mjini New York, anasimama juukwaani akishikilia ramani ya 'Mashariki Mpya ya Kati' bila Palestina.

Ramani hiyon ya 'Mashariki ya Kati Mpya' ulionyesha Ukingo wa Magharibi na Gaza ndani ya mipaka ya Israeli, jambo ambalo lilizidi kupandisha joto na fukuto la vita.

Baada ya hotuba yake, alikwenda kwenye mtandao wa kijamii wa X na kuandika, "Mafanikio makubwa zaidi katika maisha yangu ni kuwapigania ninyi watu wa Israeli na kwa ajili ya nchi yetu. Shabbat Shalom."

Kwa mujibu wa gazeti la Jerusalem Post, Netanyahu anatumia ramani hiyo kuonyesha enzi mpya ya amani katika Mashariki ya Kati ambayo ingejumuisha Palestina, hata hivyo, wakosoaji wake wakubwa wanasema kielelezo hicho kiliwasilisha mambo ambayo ni kinyume cha kile kilichokusudiwa kufanyika yaani kupatikana kwa haki ya Wapalestina ndani ya ardhi ya Mashariki ya Kati.

Yote hayo yanaitafakarisha dunia kuangalia namna bora ya kupata maridhiano na kuvumiliana baina ya Wapalestina na Waisraeli. **DW, ALJAZEERA**

## Wadau waguna ni mwenezi aliyepigwa 'X' kuingia Marekani

**INATOKA UK. 11**

Mbatia anasema ni muda mrefu hajakutana na Makonda, lakini anaamini kuwa kwa umri alinao sasa huenda atakuwa amejifunza mambo mengi na kuachana na yale aliyokuwa akifanya yaliyosababisha ajione pengine ni tofauti na wengine.

**ZIGO LA TUHUMA**

Ni hofu ya Gwandumi Mwakatobe mchambuzi wa siasa, anayesema uteuzi wa Makonda unaweza kuwa ni mkanganyiko ndani ya CCM, kwa maelezo kuwa ana tuhuma nyingi ikiwamo kukwaruzana na viongozi ndani ya chama na hata mataifa ya kigeni.

"Lakini pia anatuhumiwa kukiuka haki za binadamu na kupigwa marufuku kuingia Marekani, ninashangaa kusikia anateuliwa kushika nafasi hiyo kubwa kwenye chama," anasema Mwakatobe.

Anaongeza kuwa watu aliokosana nao ndani ya chama, kwa sasa ni mabosi wake, na kwamba inaweza kuwa vigumu kufanya naye kazi, kwa kuwa nao ni binadamu wanaumizwa kwa vitendo alivyowafanyia.

"Pamoja na hayo, suala la kuzuiwa kuingia Marekani nalo ni kubwa, yeye ni mwenezi wa chama, bado hawezi kwenda huko, kwani walimtuhumu kukiuka haki za binadamu," anakumbusha.

Anasema uongozi wa Makonda ulizua utata na kusababisha mijadala ndani na nje ya nchi hadi taifa hilo kubwa kuamua kumzuia asiingie nchini humo, na kwamba hayo na mengine yalitosha kumweka pembeni.

"Kwa maoni yangu pengine anaweza kwenda kuongeza mkanganyiko ndani ya chama, kwani sidhani yale ambayo alifanyia mabosi na viongozi wake wanaweza kufanya naye kazi kwa moyo mmoja," anasema Mwakatobe.

Itakumbukwa kwamba Marekani ilimpiga marufuku Makonda kuingia nchini humo kwa madai ya kukiuka haki za binadamu baada ya kuanzisha kampeni ya kuwasaka, kukamata na kuwashitaki watu wanaodaiwa kujihusisha na matendo ya ushoga .

Ni wakati huo Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Mike Pompeo, alipotangaza kupigwa marufuku Makonda na wanafamilia wake wa karibu kwa madai ya ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu.

Hata hivyo, hatua hiyo ya Makonda ilipingwa na serikali ikisema haihusiki na kampeni ya kuwasaka na kuwashtaki mashoga iliyotangazwa na Makonda, akieleza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi wa wakati huo, Kangi Lugola

Licha ya kwamba ushoga haukubaliki nchini tena ni jinai, serikali ilieleza kuwa kampeni hiyo haikuwa msimamo wala mkakati wake, bali maamuzi ya mkuu huyo wa zamani wa mkoa.





# Mchengerwa awatangazia neema makandarasi wazawa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa, amesema ofisi yake imeandaa mpango mkakati wa kuwezesha makandarasi wazawa ili kuwa na uwezo wa kutoa ushindani kwa wageni katika zabuni mbalimbali.

Amesema mpango mkakati huo utasaidia kuyajengea uwezo kampuni za makandarasi wazawa kuwa na ujuzi, mitaji na wataalam wenye uwezo mkubwa ili fedha zinazotolewa na serikali katika miradi zibaki nchini na kuimarisha uchumi wa maeneo husika.

Mchengerwa alisema hayo juzi jijini hapa kwenye kikao kazi kati yake na watumishi wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

Alisema akiwa katika nafasi hiyo anatamani Tanzania kuwa na makandarasi wazawa wenye uwezo ambao wataweza kushindana na kampuni za kigeni.

"Mpango huu mkakati ambao TARURA, mtausimamia ili uweze kufanikiwa natamani kila mkoa tuyajengee uwezo kampuni 20 za makandarasi wazawa na kwa mikoa yote tunaweza kuwa na kampuni 520 yenye uwezo wa ujuzi, fedha na kushindana ndani na nje ya nchi,"alisema.

Mchengerwa alisema ili kufanikisha lengo hilo TARURA, inapaswa kuanza kuchagua kampuni za wazawa ambazo zitaingia katika mpango mkakati huo.

Alisema lengo la kuwezesha makandarasi wazawa ni kupunguza matumizi ya fedha za serikali ambazo zimekuwa zikienda kwa kampuni za nje.

"Shauku yangu ni kupunguza matumizi ya fedha ambazo zimekuwa zikilipwa kwa kampuni za makandarasi wa nje ya nchi ili fedha hizo zitumike kuimarisha uchumi katika mikoa husika nchini,"alisema.

Kadhalika, alitoa maagizo kwa Mtendaji Mkuu wa TARURA kusimamia watendaji wa wakala huo ngazi ya mikoa na wilaya kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa mikataba.

Alisema hivi sasa kumekuwa na tatizo la miradi mingi kutekelezwa nje ya mkataba na chini ya kiwango hali ambayo hawezi kuifumbia macho.

Vilevile, alisema usanifu wa miradi unaofanywa uhakikishe kuwa unakamilika ili kuondoa tatizo la kuongezeka kwa kazi wakati utekelezaji unaendelea.

"Usanifu unaofanyika uhakikishe kuwa hakuna vitu vinavyoongezeka wakati mradi unaendelea kwani hali hii inatoa mianya ya rushwa na kwa ile itakayohitaji kuongezeka lazima mimi nishirikishwe,"alisema.

Mtendaji Mkuu wa TARURA, Mhandisi Victor Seif alisema watayafanyia kazi maelekezo yote yaliyotolewa na waziri ili kuongeza tija katika wakala huo.

# MSD yasambaza vyandarua 341,000 shule za msingi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

BOHARI ya Dawa (MSD) imeanza kusambaza vyandarua 341,000 katika shule za msingi zilizopo katika halmashauri sita za Mkoa wa Singida.

Lengo likiwa ni kuhakikisha malengo ya taifa ya kutokomeza malaria ifikapo mwaka 2030 yanatimia.

Meneja wa MSD Kanda ya Dodoma, Mwanashehe Jumaa, aliyasema hayo wakati akizungumza kwenye uzinduzi na uhamasishaji wa kampeni ya ugawaji wa vyandarua kwa shule za msingi za Mkoa wa Singida, akisema zoezi hilo litachukua wiki tatu kukamilika.

Alisema, MSD imepewa jukumu la kusambaza vyandarua hivyo kutokana na uzoefu wa kusambaza dawa na vifaa tiba nchini na uwepo wa miundombinu ya usafiri na miundombinu ya kielektroniki.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema serikali zote kuanzia awamu ya kwanza hadi ya sita imekuwa na malengo ya kupambana na malaria kwa kuwakinga wananchi dhidi ya ugonjwa huo kwa kuwagawia vyandarua vyenye dawa bila malipo.

Alisema ugonjwa wa malaria bado ni tatizo katika Mkoa wa Singida kutokana na utafiti uliofanyika mwaka 2022 ukionesha kiwango cha maambukizi ya ugonjwa huo kuwa ni asilimia 1.5.

Serukamba alisema kutokana kiwango hicho cha maambukizi serikali imeendelea kuchukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na ugawaji wa vyandarua, kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Njia nyingine zinazotumika katika kuhakikisha serikali inatokomeza malaria ifikapo mwaka 2030 ni kuimarisha ufuatiliaji na tathimini ya mipango ya malaria kitaifa unalenga kuwa na maambukizi chini ya asilimia 3.5 ifikapo mwaka 2025 na kuhamasisha jamii juu ya afua mbalimbaliza udhibiti wa malaria.

Kadhalika, Serukamba aliziagiza halmashauri kutenga fedha katika mapato yao kwa ajili ya kununulia dawa za kuulia mazalia ya mbu na kuagiza kila mwanafunzi atakayepewa chandarua kitumike kwa matumizi sahihi ili kuendeleza mapambano dhidi ya malaria.

Mwakilishi wa Meneja wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kutoka Wizara ya Afya, Theresia Shirima, alisema wananchi wahakikikishe wanavitumia vyandarua hivyo kwa malengo yaliyokusudiwa na halmashauri zitunge sheria ndogo kudhibiti watakaovitumia kinyume cha malengo yaliyokusudiwa.

Shirima alisema mikoa ya Tabora, Mtwara, Kagera na mikoa ya kusini kiwango cha maambukizi ya malaria kipo juu.



Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Prof. Jamal Katundu (kushoto) na Mkurungenzi wa Kampuni ya Su-Yapi Engineering Consulting Inc, Mhandisi George Sarkis wakitiliana saini jijini Dodoma jana, mkataba wa ujenzi wa bwawa la maji la Furkwa wilayani Chemba, utakaogharimu sh. bilioni 312 kwa awamu ya kwanza. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Aweso aziagiza mamlaka za maji kuwashirikisha wananchi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso amewataka mamlaka za maji nchini kuwashirikisha wananchi kuhusu fursa na faida za uwepo wa miradi ya maji kwenye maeneo yao.

Aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye hafla ya utiaji saini mkataba wa usanifu wa ujenzi wa bwawa la maji Farkwa Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma.

Alisema ujenzi wa bwawa hilo utakapokamilika utakuwa na maji ya kutosha ambapo wananchi wa maeneo hayo watapata fursa ya kuendesha kilimo cha mazao mengi.

Waziri Aweso alibainisha kuwa mradi huo ambao ulisainiwa jana kati ya Serikali na Kampuni ya Su -Yapi Engineering Consulting Inc unatarajiwa kukamilika mwaka 2025.

Aweso alisema mradi huo utasaidia kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa makao makuu ya nchi inayotolewa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA) .

Pia, alisema uwapo wa miradi hiyo ya maji kwenye maeneo husika wananchi wataweza kuyatumia maji hayo kuzalisha mazao ya mboga na chakula na kupunguza hali ya umaskini kwenye maeneo hayo.

Alisema wananchi wa maeneo ya vijiji vilivyopo jirani na mradi huo watakuwa wa kwanza kupata huduma ya maji, ndipo ili kunufaika na mradi huo .

Waziri Aweso alisema miradi hiyo inayoanzishwa na serikali mali ya wananchi, hivyo wanatakiwa kushirikishwa ili kunufaika kiuchumi wa maeneo husika.

Aidha, alieleza kuwa mkakati wa muda mfupi walionao kuhusu upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma ni kuchimba visima vya maji kwenye maeneo ya pembezeni.

Awali, Kaimu Mkurungenzi Mtendaji wa DUWASA, Lena Mwakisale alisema kwa sasa wanategemea vyanzo vya maji ya visima virefu vilivyopo Bonde la Makutupora eneo la Mzakwe na wanazalisha maji lita milioni 68.6 kwa siku na mahitaji ni lita milioni 133 kwa siku.

Mwakisale alisema kuna mradi wa visima vitano unatarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni na utakuwa na uwezo wa kuzalisha lita kuhudumia wananchi waishio maeneo ya Nzuguni, Ilazo, Kisasa na Ipagala.

Akielezea utekelezaji wa mradi huo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji ,Mhandisi Mwajuma Waziri alisema mradi huo unatekelezwa kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) kwa mkopo wa masharti nafuu kwa Dola za Marekani milioni 125.3 na mkataba huo ulisainiwa Mei 16, Mwaka 2022.

Alisema ujenzi wa bwawa hilo itakuwa urefu wa mita 32 na ujenzi wa mtambo wa kusafirisha maji wenye uwezo wa kusafirisha lita 128,000 kwa siku.

Aliongeza kuwa watapanda miti ekari 75 na watatoa mafunzo kwa vikundi 200 vya kutunza mazingira kuzunguka eneo la bwawa.





# Serikali kufungua mipaka uuzaji mazao kimataifa

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

SERIKALI imesema itaendelea kufungua mipaka ili kuuza bidhaa za mazao nje ya nchi kwa sababu bado kuna Watanzania hawajatumia vema Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliyasema hayo wakati akifungua maonesho ya nne ya viwanda vidogo vidogo kitaifa mkoani Njombe.

Alisema ni jukumu la watu wote kuhakikisha wanaunganisha kilimo na viwanda ili kutumia ipasavyo fursa za masoko.

"Niwahakikishie kuwa iwapo tutaunganisha kilimo na viwanda tutaweza kukuza soko la ndani pia kupunguza uagizaji bidhaa ambazo tunaweza kuzizalisha sisi wenyewe kutokana na mazao ya kilimo na malighafi nyingine ambazo tunaweza kuzalisha ndani," alisema.

Kigahe alisema serikali imejipanga kuhakikisha inalisha dunia na Afrika kwa bidhaa ambazo zimeongezwa thamani.

"Siyo kuuza nje parachichi kama ilivyo kuuza mahindi kama yalivyo, alizeti na mengineyo, tuuze unga, tuuze bidhaa zilizoongezwa thamani, tuwalishe chakula ambacho kimeongezwa thamani kutoka Tanzania" alisema Kigahe.

Aidha, alilitaka SIDO kushirikiana na halmashauri ili kuhakikisha vijana wanapata teknolojia ili kuweza kufanya kilimo kibiashara.

Meneja Uhusiano Mwandamizi huduma za benki kwa serikali NMB, Josephine kulwa, alisema maonesho hayo ni fursa kwa wajasiriamali wadogo na wafanyabiashara mkoani Njombe ili kupata elimu ya mambo mbalimbali ikiwemo huduma zinazotolewa na Benki ya NMB.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa alimshukuru Rais Samia kwa kutoa ruzuku kwenye mbolea ili kuongeza uzalishaji kwenye mazao ya chakula.

Mkurugenzi wa SIDO, Prof. Sylivester Mpanduji, alisema wamejipanga kutoa elimu kupitia simu za mkononi ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi ambao watahamasika kuanzisha viwanda.

Msaidizi wa Usajili Mwandamizi Kurugenzi ya Miliki Ubunifu kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Nassoro Mtavu, alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya huduma ya usajili wa majina ya biashara.




Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, ACP Benjamin Kuzaga akiwaonyesha waandishi wa habari, baadhi ya pikipiki za magurudumu matatu (bajaji) zilizokamatwa zikitumika kwenye matukio mbalimbali ya uhalifu zilizohifadhiwa katika Kituo cha Polisi cha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mbaroni kumiliki gobole bila ya kibali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya linamshikilia mzee mmoja aitwaye Pascal Mwango (80) mkazi wa Kijiji cha Madundasi Wilaya ya Mbarali mkoani humo kwa tuhuma za kumiliki bunduki aina ya gobole bila kuwa na kibali huku akiitumia kwa ujangili.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi Benjamin Kuzaga alisema mtuhumiwa alikamatwa Oktoba 20 mwaka huu katika eneo liitwalo Masenjele ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa kufuatia msako maalumu uliofanywa mna maofisa wa Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Askari wa Jeshi la Uhifadhi (Jeshi USU) ambao walikuwa kwenye doria ya kuwasaka wawindaji haramu ndani ya hifadhi hiyo.

Kamanda Kuzaga alisema mzee huyo alipopekuliwa alikutwa na bunduki hiyo, risasi (golori) 35, unga wa baruti ukiwa kwenye mfuko wa plastiki, kisu kimoja, kiberiti na fataki mbili za kulipulia bila vitu ambavyo alikuwa anamiliki bila kuwa na vibali.

"Mtuhumiwa amekuwa akifanya uhalifu kwa kuwinda na kuua wanyamapori ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, kwahiyo tunaendelea kumshikilia na upelelezi unaendelea wakati tukijiandaa kumpeleka mahakamani," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema Jeshi la Polisi lipo kwenye kampeni maalumu ya msamaha wa usalimishaji silaha haramu kwa hiari iliyoanza Septemba Mosi na inatarajiwa kumalizika Oktoba 31, 2023 mwaka huu.

Aliwataka wananchi wote wanaomiliki silaha kinyume cha sheria kusalimisha kwa hiari katika vituo vya polisi, ofisi za serikali za mitaa na ofisi za watendaji wa kata.

## Watoto 300,000 kupimwa polio awamu ya pili Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATOTO zaidi ya 300,000 wenye umri wa chini ya miaka nane wanatarajiwa kupatiwa chanjo ya polio awamu ya pili kwa siku tatu kuanzia Oktoba 26 wilayani Mbeya.

Mratibu wa chanjo wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Christopher Msaghaa aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa chanjo hiyo, kusema watoto hao wamegawanyika kwenye halmashauri zote mbili za wilaya hiyo.

Alisema kwa Jiji la Mbeya wanatarajia kuchanja zaidi ya watoto 168,000 na kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wanakusudia kuchanja zaidi ya watoto 131,000 na kwamba watatembelea kata zote za wilaya hiyo.

Alisema ili kufanikisha zoezi hilo wanakusudia kutembelea maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko ya watoto ikiwemo kwenye shule za msingi na awali, vituo vya kulelea watoto yatima, kwenye taasisi za dini na majumbani.

"Tutachanja pia maeneo mengine ambayo wanajamii watayabainisha kwamba kuna watoto wenye umri lengwa, chanjo hii ni muhimu sana kwahiyo tunaomba wananchi watupe ushirikiano kama ambavyo ilikuwa awamu ya kwanza," alisema Dk. Msaghaa.

Mwakilishi wa Wizara ya Afya, Penford Joel alisema serikali iliamua kutoa chanjo hiyo pamoja na chanjo ya magonjwa mengine ya mlipuko kutokana na kuwepo kwa mwingiliano wa watu kutoka mataifa mbalimbali.

Alisema Tanzania inapakana na baadhi ya mataifa ambayo yamekuwa yakikabiliwa na milipuko ya magonjwa hayo ukiwemo ugonjwa wa polio ambao ni miongoni mwa magonjwa hatari kwa watoto.

Aliwaomba viongozi wa maeneo mbalimbali kuhakikisha wanawahamasisha wananchi kuwapeleka watoto wao kwenye vituo vya kutolea chanjo ili kukabiliana na magonjwa hayo.

"Tunaweza tukawa tunapambana na polio kumbe surua nayo imo, kwahiyo naomba tuhakikishe tunawahamasisha wananchi wetu, mkoa huu wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa iliyoko mipakani kwahiyo lazima tuwekeze nguvu kubwa," alisema Penford.

Aliwataka wataalamu watakaoshiriki kwenye chanjo hiyo kuhakikisha wanapita nyumba kwa nyumba ili asiachwe mtoto yoyote kwenye chanjo hiyo.

Akizindua kampeni hiyo ya chanjo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Benno Malisa aliagiza kufanyika maboresho ili dosari zilizojitokeza kwenye chanjo ya awamu ya kwanza zisijirudie.

Alisema wakati wa chanjo ya awamu ya kwanza kuna baadhi ya maeneo hayakufikiwa na hivyo akawataka maofisa hao kuanza na maeneo hayo kabla ya kuendelea na maeneo mengine.

Meya wa Jiji la Mbeya, Shekhe DorMohamed Issa alishauri viongozi wa serikali za mitaa washirikishwe ili washiriki vizuri kwenye uhamasishaji wa chanjo hiyo.

Alisema viongozi hao ndio walioko jirani na wananchi na hivyo ni rahisi kuwafikia kwa wakati mfupi tofauti na kuwatumia viongozi wa ngazi za juu pekee.





# Dk. Mwinyi: Msongamano wa wanafunzi bado tatizo Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema kuwa Zanzibar inakabiliwa na tatizo kubwa la idadi ya wanafunzi madarasani, hali ambayo imesababisha wanafunzi kutofundishwa vizuri.

Aliyasema hayo visiwani Zanzibar wakati akiweka jiwe la msingi katika Shule ya Ghorofa Donge iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja ikiwa ni miongoni mwa shamrashara za kuhitimisha miaka mitatu ya uongozi wake.

Dk. Mwinyi alisema kutokana na wingi wa wanafunzi hao wanalazimika kwenda shule kwa zamu, nyakati za asubuhi na mchana.

Alisema kasi ya ujenzi wa shule inakwenda kutatua changamoto hiyo katika muda mfupi ujao, kwamba wanafunzi wataanza kusoma kwa wakati mmoja.

Dk. Mwinyi alisema dhamira ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuona kila darasa halizidi wanafunzi 45, ili kiwango cha elimu nchini kipande.

Aidha, alisema kasi hiyo ya ujenzi wa shule inakwenda sambamba na kuajiri wa walimu hasa walimu wa sayansi na hesabati, ili kiwango cha elimu kiwe bora zaidi na vijana kuelimika vizuri na kuwasaidia katika maisha yao ya baadae.

Dk. Mwinyi alisema tayari Zanzibar imevuka malengo ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM Mwaka 2020-2025 katika sekta ya elimu kwa kujenga shule 29 za ghorofa.

"Ifikapo kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 wapinzani wetu watakuwa hawana la kusema katika majukwaa ya mikutano ya hadhara kwa sababu mambo yote ya msingi na muhimu yamefanywa na Chama Cha Mapinduzi" alisema.

Katika hatua nyingine, Dk. Mwinyi aliweka jiwe la msingi Shule ya Sekondari Munduli na Shule ya Muembeladu katika Mkoa wa Mjini magharib Unguja.

Alisema ameridhishwa na kasi ya jenzi wa shule hiyo inayojengwa na Jeshi la Magereza baada ya serikali kumuondoa mkandarasi wa awali aliekuwa akijenga shule hiyo ambapo ujenzi wake ukisuasua.

Dk. Mwinyi alisema majengo kama hayo yanahitajika mengi ili kuondosha tatizo la msongamano la wananfunzi madarasani, kwa sababu katika uhai wa binadamu hakuna jambo zuri kama elimu.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, alisema lengo la kasi ya utekelezaji wa miradi ya elimu ya ujenzi wa shule ni kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

Alisema Shule ya Msingi Donge itakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,305 hatua ambayo itapunguza msongamano wa wanafunzi kutembea zaidi ya kilomita mbili kutafuta elimu.

Kwa upande wa Shule ya Sekondari Munduli, alisema ndani ya miaka mitatu ya uongozi wa Dk. Mwinyi ameshajenga madarasa 2,375 kati ya madarasa 525.



Wafanyakazi wa KFC, wakiwahudumia chakula watoto wakati wa sherehe za maadhimisho ya miaka 10 ya kampuni hiyo nchini, jijini Dar es Salaam juzi. Hafla hiyo, ilihudhuriwa na watoto 50 pamoja na walezi 10 kutoka Taasisi ya Baba Oreste, pamoja na watoto 50 na walimu 6 kutoka Shule ya Msingi na Awali ya Rightway. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Makamu wa Rais atoa maagizo Baraza la Chake Chake Pemba

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla ameutaka uongozi wa Baraza la Mji la Chake Chake Pemba kuhakikisha wanasimamia vyema vyanzo na ukusanyaji mzuri wa mapato ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Aliyasema hayo wakati akizindua Baraza la Manispaa hilo na kumpongeza Dk. Mwinyi kwa kasi kubwa ya kuimarisha utendaji kazi katika serikali za mitaa na kuridhia mapendekezo ya kulipandisha hadhi Baraza la Mji Chake Chake na kuwa Baraza la Manispaa kwa kuzingatia Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Alisema kuwa matarajio ya serikali ni baraza hilo jipya litahakikisha huduma za kijamii zinakuwa bora na za ufanisi zaidi ambazo zitawaondolea usumbufu wananchi kwa kupata huduma pamoja na kuandaa mipango bora ya kimkakati itakayotoa tija kwa wananchi na serikali.

Aidha, aliwataka watendaji wa baraza hilo kusimamia vyema makusanyo kwa kutumia mifumo ya risiti za kielektroniki, kuwa na matumizi sahihi ya rasilimali watu na rasilimali fedha, kuibua miradi ya maendeleo, kuimrisha usafi wa mazingira na kusimamia amani na mshikamano katika jamii.

Pia, aliwataka watendaji wake kukemea vitendo vya rushwa na utumiaji mzuri wa rasilimali za serikali, kuacha uhali na kutanguliza maslahi ya taifa ili kuwa baraza la mfano.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohamed aliwataka watendaji wa baraza hilo kwa kushirikiana na wananchi kuongeza kasi katika utendaji wa kazi kuwa wabunifu wa miradi itakayowaongezea kipato.

Alisema ushirikiano ndio silaha katika kutimiza majukumu yao ya kazi na kuachana na kufanya kazi kwa utashi binafsi na kuelekeza nguvu zao katika kulitumikia taifa.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mattar Zahor Massoud alisema aliwataka viongozi kufanya kazi kwa pamoja hasa katika shuhuli za maendeleo na kuachana na tabia ya kukwamisha na kuzorotesha miradi ya maendeleo.

Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa Chakechake, Maulid Mwalim Ali, alisema kupandisha hadhi kwa baraza hilo kutawajengea ari na morali wafanyakazi katika kufanya kazi kwa umakini na weledi.

Alisema baraza litahakikisha linaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kuimarisha usafi wa mazingira na kuendelea kutekeleza miradi ya kimaendeleo pamoja na kuwapatia elimu zaidi wafanyakazi ili kuleta ufanisi mzuri wa kazi.

## Ujenzi barabara za vijijini kuimarisha sekta ya utalii Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imesema ujenzi wa barabara za vijijini (Km 275.5) utaimarisha sekta ya utalii na kuiunganisha mikoa ya Zanzibar katika miundombinu ya barabara.

Hayo yalisemwa na wizara hiyo, Dk.Khalid Salum Mohamed alipotembelea ujenzi wa barabara zinazokwenda vijijini Unguja na Pemba ambazo zinajengwa na kampuni kutoka Uturuki.

Alisema Serikali ya Zanzibar imejipanga kuimarisha miundombinu ya barabara zinazokwenda vijijini ikiwemo katika miradi ya hoteli za kitalii.

Aidha, alisema Sh.bilioni 373.54 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo ambazo zitajengwa kwa kiwango cha lami na kufika katika maeneo ya miradi ya hoteli za kitalii.

Alizitaja baadhi ya barabara ambazo zimejumuishwa na kuhusishwa na ukarabati mkubwa ni Fumba hadi Kisauni Wilaya ya Magharibi Unguja pamoja na Makunduchi hadi Tunguu Wilaya ya Kati Unguja.

"Tumeanza ujenzi wa barabara za ndani zinazokwenda katika mikoa ya Kusini na Kaskazini Unguja na Pemba ambazo zitafika katika maeneo ya sekta ya utalii na miradi ya hoteli" alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini Unguja, Sadifa Juma Khamis, alisema ujenzi wa barabara za ndani kwa kiasi kikubwa utasaidia na kurahisisha huduma za usafiri kwa wananchi pamoja na watalii.

Alisema katika Jimbo la Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja ujenzi wa barabara za ndani ni muhimu ili kurahisisha huduma za usafirishaji kwa watalii.

**Alizitaja baadhi ya barabara ambazo zimejumuishwa na kuhusishwa na ukarabati mkubwa ni Fumba hadi Kisauni Wilaya ya Magharibi Unguja pamoja na Makunduchi hadi Tunguu Wilaya ya Kati Unguja.**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ERICA MOSES CHAWE** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba S.1093/0570 iliyotolewa na **ALDERSGATE SEKONDARI** mwaka 2023. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/ILA/29728/202**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JASMINE HASSAN GULEID** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 711 DZU – NISSAN X-TRAIL.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/5146/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARK MICHAEL NTABAGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0165/0041 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **URU SEMINARY** mwaka **2017.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/29944/2023.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**GILPHINE KARUMUNA EDGARD** anatangaza kupotea kwa **RESULT SLIP** ya kidato cha sita yenye index namba **S0686/0604/2023** iliyotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **CHATO SEKONDARI** mwaka 2023. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/UBU/29913/2023**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIGOMA AT KIGOMA**

**(EXTENDED JURISDICTION)**

**(PC) CRIMINAL APPEAL NO. 1 OF 2023**

**(From original Criminal Case No. 181/2022 Kasulu District Court at Kasulu)**

**EZEKIEL NKEZIDYO……………………………1st APPELLANT**

**DOGO HAMIS……………………………………2nd APPELLANT**

**LIBERATUS CHIJA……………………………3rd APPELLANT**

**VERSUS**

**ABEL HOZE………………………………………RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE OF HEARING**

**TO: ABEL HOZE**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for Hearing on 06th day of NOVEMBER, 2023 AT 09:00AM Before **Hon. R.E. KANGWA, PRM EXT.J.**

YOU ARE required to appear in this Court on the fixed date without fail.

**GIVEN UNDER MY HAND** and the **SEAL** of the Court, this 19th day of OCTOBER.

RESIDENT MAGISTRATE

COPY TO BE SERVED UPON

……………………………

Signature ……………………

Date ……………………

**FOMU MADAI No-3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**

**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa wa GEITA**

**Shauri la Madai Na. 150/2023.**

**JINA LA MDAI: PE-RENA MICROFINANCE CO. LTD**

**JINA LA MDAIWA: DAMIAN LUCAS**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu za mashauri ya madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: DAMIAN LUCAS**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**

**MADAI YA FEDHA TSH. 500,000/- ZA MKOPO**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 27 Mwezi wa 10 Mwaka 2023 saa 2:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na kupigwa Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 18 Mwezi wa 10 Mwaka 2023.

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE
GEITA.

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA WILAYA SONGWE**
**LILILOPO MBOZI**
**SHAURI NA.31/2022**
**HIDAYA BATAZA KONZO:::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**1.ESSAU KABUJE::::::::::::::::::::MDAIWA**
**2.SALOME W.SEME::::::::::::::::MDAIWA**
**3.ELIA HEMRE MHELELA::::::::::MDAIWA**

**YAH:KUITWA SHAURINI**
**KWA: ESAU S.KABUJE,SALOME W.SEME,**
**ELIA HEMRE MHEMELA**

Fahamu kwamba **HIDAYA BATAZA KONZO** amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.

Shauri limepangwa kusikilizwa tarehe **27/10/2023 saa 2:30** asubuhi mbele ya **Mhe.T.Munzerere**, Mwenyekiti wa Baraza.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Mnadani-Vwawa.

Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo hukumu itasomwa pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 12/10/2023.

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**12/10/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 106 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late YASINTA BRUNO GELLE of Ukombozi - Chamwino District within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY THERESIA BRUNO GELLE**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **25 Day of 10,2023**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA CHETI



**GEORGE WILLIAM KAPINGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4645/0023** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ALLIANCE BOYS' SEKONDARI** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KNY/RB/1222/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NEEMA KAMARA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S2652/0043/2015** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KOM SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/9801/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMANUEL ARBOGAST KWEKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 450 CFW - TOYOTA VITZ. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya **Polisi: TAR/RB/454/2023.**

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701***

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mateka asimulia maisha chini ya mahandaki

- Ni baada ya kuachiliwa wengine wawili
- Wadai Hamas waliahidi kutowadhuru



Mmoja wa mateka raia wa Israel Yocheved Lifshitz (85) aliyeachiwa na kundi la Hamas, jana. **PICHA: MTANDAO**

**TEL AVIV,** Israel

BAADA ya kundi la wanamgambo wa Hamas kuwaachia huru mateka wawili raia wa Israel, mmoja wao amesimulia namna walivyokuwa wakiishi kwenye mahandaki huko Gaza chini ya uangalizi wa kundi hilo, na kurudisha matumaini juu ya usalama wa ambao hawajaachiliwa.

Kwa mujibu wa taarifa ya ofisi ya Waziri Mkuu wa Israel mateka hao walioachiliwa usiku wa jana chini ya msaada wa Shirika la Msalaba Mwekundu ni wanawake wawili, Nurit Cooper, mwenye umri wa miaka 79 na Yocheved Lifshitz (85).

Akielezea hali halisi ilivyokuwa Yocheved Lifshitz (85), alisema alitekwa nyara kutoka kwenye nyumba yake, na kwamba alipigwa kwa fimbo, na kushikiliwa kwenye mahandaki chini ya Gaza kwa wiki mbili, kabla ya kuachiliwa jana usiku.

Yocheved alielezea mazingira ambayo yeye na mateka wenzake waliwekwa, akisema yalikuwa safi. Na kwamba walilala kwenye magodoro sakafuni kwenye mahandaki chini ya uangalizi wa Gaza, huku daktari akipita kuwatembelea kila baada ya siku mbili hadi tatu.

"Mateka ambaye alijeruhiwa vibaya katika ajali ya pikipiki akiwa njiani kuelekea Gaza alitibiwa majeraha yake," alisema Yocheved.

Aliongeza kuwa mhudumu wa afya alifika kuwaona ili kuwaletea dawa walizohitaji, akieleza kwamba alipitia makubwa na alipata michubuko alipokuwa akitekwa nyara kutoka kwenye makazi yake huko Israel.

> Wakati hayo yakijiri, pia ilibainishwa kuwa licha ya hospitali za Gaza kupungukiwa na mafuta ya kuendesha jenereta wodi mbili za watoto katika hospitali mbili zina wasiwasi na hali mbaya kutokana na kukosekana kwa umeme.

Akisaidia kutoa simulizi ya mama yake, binti yake Sharone ambaye aliwasili mjini Tel Aviv kutoka London asubuhi ya jana, alisema Lifschitz na mateka wenzake walipigwa kwa fimbo.

Sharone pia alisema mama yake alishuhudia mtandao mkubwa wa mahandaki chini ya ardhi yanayoendeshwa na Hamas, ambao aliufananisha na utando wa buibui.

Sharone alisema baada ya kufika Gaza, watekaji wa mama yake walisema wanaamini katika Quran (maandiko ya dini ya Kiislam) hivyo hawatamdhuru.

Lifschitz mwenyewe aliendelea kuelezea hali safi na walinzi ambao walitunza kila undani. Na kwamba walilishwa ibini nyeupe na tango chakula ambacho watekaji pia walikila.

Akizungumzia mateka wengine waliochukuliwa na Hamas, Sharone alisema mama yake alihisi hadithi haijaisha hadi kila mtu arudi.

Kamati ya kimataifa ya msalaba mwekundu ilisema ilisimamia kuachiwa huru kwa mateka hao na kwamba liko tayari kuendelea kufanya jukumu hilo katika siku za usoni, huku Hamas ikisema limewaachia huru wafungwa hao kwa sababu za kibinadamu.

**KAULI YA ISRAEL**

Aidha, Israel imetaka kuachiliwa huru bila masharti mateka wote wanaoshikiliwa na kundi la Hamas ambalo linaorodheshwa kama la kigaidi na Israel, Umoja wa Ulaya (EU), Marekani na mataifa mengine ya magharibi.

Jeshi la Israel lilisema jana kwamba watu takribani 222 walitekwa nyara na kupelekwa Gaza, wakiwemo raia wa kigeni.

Renana Gomeh Muisraeli, ambaye ni mama wa mateka wawili wanaozuiliwa na Hamas, alisema hana taarifa yoyote kuhusu hali za watoto wake, na kwamba mawasiliano ya mwisho aliyokuwa nayo na vijana wake kwa njia ya simu ilikuwa muda mfupi kabla ya kutekwa na Hamas na kupelekwa Gaza, na hajui waliko, au ikiwa wangali hai.

**VITA VISITISHWE**

Mwanadiplomasia Mkuu wa EU, Josep Borell, alitoa wito kwa pande zote mbili kusitisha vita katika ukanda wa Gaza kwa sababu za kibinadamu.

Akizungumza baada ya kukutana na mawaziri wa mambo ya nje wa EU mjini Luxembourg jana, Borell alisema anaamini wazo la kusitisha vita kuratibu kuwasili kwa msaada wa kiutu, utakaowaruhusu watu waliolazimika kuyakimbia makazi yao kupata hifadhi, ni jambo ambalo viongozi wataliunga mkono.

Pia alisema hatua hiyo haipiti lengo la kuwa na kipindi cha utulivu kwa sababu za kibinadamu kilichoitishwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio Guterres. Huku wito huo ukiungwa mkoano na mawaziri kadhaa wa EU.

**HOSPITALI ZAZIDIWA**

Wakati hayo yakijiri, pia ilibainishwa kuwa licha ya hospitali za Gaza kupungukiwa na mafuta ya kuendesha jenereta wodi mbili za watoto katika hospitali mbili zina wasiwasi na hali mbaya kutokana na kukosekana kwa umeme.

Mkurugenzi wa Hospitali ya al-Aqsa, Iyad Abu Zahar, iliyoko mji wa Deir al-Balah katikati ya Ukanda wa Gaza alionyesha wasiwasi kwamba watoto kutoka kwenye wodi hizo huenda wakafa mara tu jenereta zitakapozima, kutokana na kuishiwa mafuta, akisisitiza kuwa jukumu walilonalo ni kubwa.

Wafanyakazi wa kutoa misaada walisema watoto takribani 130 waliozaliwa kabla ya wakati wao kufika, wanakabiliwa na kitisho kikubwa katika vituo sita vya watoto.

Msemaji wa Wizara ya Afya inayoendeshwa na Hamas katika ukanda wa Gaza, Ashraf al-Qidra, alisema hospitali zinapungukiwa na mafuta na wanatumia mafuta kwa huduma muhimu pekee za kuokoa maisha, ikiwemo kuendeshea mashine za watoto waliozaliwa mapema kabla ya wakati, lakini hawafahamu wataendelea kufanya hivyo kwa muda gani.

**UGAIDI UKOMESHWE**

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Annalena Baerbock, alisisitiza umuhimu wa kupambana na ugaidi wa kundi la Hamas, ambalo limeorodheshwa kuwa la kigaidi nchini Ujerumani, Marekani na EU.

Katika kauli aliyoitoa kabla ya ziara yake ya kwenda New York, Marekani, Baerbock alisema haiwezekani kuwa na usalama wakati kukiwa na ugaidi wa Hamas, sio tu kwa Israel bali pia kwa Wapalestina.

Pia aliituhumu Hamas kwa kutaka kuchochea chuki katika jamii kote ulimwenguni, sio tu katika ulimwengu wa kiarabu. Akisisitiza kuwa msaada wa wakazi wa Gaza unatakiwa uendelee kutolewa kupitia kwa UN na kutoa wito wa kuwepo mazingira yatakayowawezesha wafanyakazi wa misaada wa umoja huo kutoa misaada katika ukanda wa Gaza.

"Suluhisho la mataifa mawili linaweza kuleta maisha ya amani baina ya Waisraeli na Wapalestina," alisema Baerbock.

**VIFO VYAFIKIA 5,300.**

Wakati wito wa kusitisha mapigano ukitolewa Wizara ya Afya ya Palestina katika Ukanda wa Gaza ilisema jana kuwa idadi ya vifo katika ukanda huo tangu kuanza kwa vita kati ya Hamas na Israel imeongezeka na kufikia watu 5,300 huku watu wengine 18,000 wakijeruhiwa.

Mkurugenzi wa hospitali za Ukanda wa Gaza, Muhammad Zaqout, alisema katika kipindi cha saa 24 zilizopita, hospitali hizo zilipokea watu 120 waliofariki na wengine kadhaa waliojeruhiwa.

Alieleza kuwa wahudumu 17 waliokuwa wakifanyakazi ya kuwasafirisha majeruhi waliuawa, na kwamba magari 25 ya kubebea wagonjwa pia yameharibiwa. **BBC, DW**

HABARI MICHEZO

# JKT TANZANIA, TABORA UNITED NA VITA CHAMPIONSHIP LIGI KUU LEO

Na Saada Akida

LIGI Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea leo ambapo nyasi za viwanja vitatu zitawaka moto kwa timu sita kumenyana ikiwamo JKT Tanzania watakaowakaribisha Tabora United.

Mchezo huo utapigwa majira ya saa nane mchana kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, huku mechi nyingine ikizikutanisha Coastal Union na Mashujaa FC katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Mechi nyingine itakuwa kati ya wenyeji, Dodoma Jiji FC wakiwakaribisha Kagera Sugar katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

**Kwa upande wa JKT Tanzania ambayo ipo nafasi ya tisa ikiwa na pointi nane, inakutana na Tabora United iliyopo nafasi ya tano na alama tisa katika msimamo wa ligi hiyo, ambapo zote zimeshuka dimbani mara sita hadi sasa.**

Timu hizo hii inakuwa ni mara ya tatu kukutana, mara mbili zilikutana mechi ya Ligi ya Championship ambapo mchezo wa kwanza JKT Tanzania walishinda mabao 3-1 nyumbani na mechi ya pili Tabora United walishinda 2-1.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Msaidizi wa JKT Tanzania, George Mketo, alisema maandalizi yanaendelea vizuri na tayari wao kama benchi la ufundi wamemaliza majukumu yao na kazi kubwa imebaki kwa wachezaji kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

Alisema wanajiandaa vizuri kulingana na ubora wa Tabora United na kutaka kufanya vizuri katika mchezo huo ili kujiweka kwenye nafasi za juu.

"Tutakuwa nyumbani, mchezo utakuwa mgumu, lakini tumejiandaa vizuri wachezaji wako tayari kwa ajili ya kutafuta alama tatu muhimu," alisema Mketo.

Mwakilishi wa wachezaji wa JKT Tanzania, Hassan Kapalata alisema wako tayari kwa mchezo huo na mechi inaugumu wake kwa sababu ya kujuana kwa kuwa wametoka wote katika Ligi ya Championship.

Alisema Tabora United ya sasa haitakuwa ile ambayo waliwahi kucheza nayo kwa sababu ya kuwa na benchi jipya na kujiimarisha zaidi kwa ajili ya kupambana katika Ligi Kuu na kwamba watakuwa wamejipanga kupata alama tatu muhimu.

"Haitakuwa mechi rahisi kwa sababu kila timu imejiandaa vizuri, tuliwahi kukutana katika Ligi ya Championship ila mechi ya kesho (leo), ni tofauti kabisa, hii ni ligi na tunahitaji kutafuta alama tatu muhimu ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo," alisema Kapalata.

Kwa upande wa Kocha wa Tabora United, Goran Kopunovic, alisema wamejiandaa vizuri na wako tayari kutafuta alama muhimu katika mchezo huo.

"Ni mechi muhimu kwetu, tunahitaji kufanya vizuri ili kuendelea kuwapo katika nafasi za juu kwenye msimamo, utakuwa mchezo wa mbinu na kiufundi kulingana na timu kujuana ubora na madhaifu yao," alisema Goran.

BURUDANI...



Wasanii wa Ngoma za Asili wa Kundi la Msanii Theatre, wakitoa burudani jana katika mkutano wa kimataifa wa siku tatu wa Mabibi unaoendelea katika viwanja vya Msimbazi Centre jijini Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

## *Katwila na mtihani wa kwanza Mtibwa kesho*

Na Adam Fungamwango

MTIHANI wa kwanza kwa kocha mpya wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, utaanza kesho atakapoiongoza kwenye mechi dhidi ya Geita Gold, Uwanja wao wa Manungu Complex uliopo Turiani mkoani Morogoro.

Mtibwa Sugar ilimtangaza rasmi juzi kocha huyo kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Habib Kondo aliyeoneshwa mlango wa kutokea baada ya matokeo mabaya katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Katwila, straika wa zamani wa timu hiyo, alijiuzulu kwenye timu yake aliyokuwa akiifundisha zamani, Ihefu FC, ikiwa ni siku chache baada ya kuifunga Yanga mabao 2-1 Oktoba 4, na kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Ihefu, Oktoba 7, mwaka huu.

Wakati anaondoka Ihefu, tayari kulikuwa na minong'ono ya kuelekea Mtibwa Sugar kabla hata ya kutangazwa rasmi.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thobias Kifaru, amesema wana uhakika kikosi chao kitabadilika kiuchezaji kutokana na mbinu za mwalimu huyo ambaye anajua falsafa ya klabu hiyo.

"Amerudi nyumbani, hatuna wasiwasi naye, alikuwa straika wetu kwa hiyo anaijua Mtibwa Sugra nje na ndani, naamini atatusaidia kwenye kipindi hiki kigumu," alisema Kifaru.

Zuberi tayari ameanza kazi ya kukinoa kikosi hicho na kesho ataisimamia timu hiyo kwa mara ya kwanza wakati ikicheza nyumbani dhidi ya Geita Gold.

Kazi aliyonayo ni kuhakikisha inapata ushindi wa kwanza, kwani mpaka sasa licha ya kuburuza mkia, haijashinda mechi yoyote ya Ligi Kuu ikicheza michezo sita, sare mbili na kupoteza nne, ikiweka rekodi mbaya msimu huu ya kupoteza mechi tatu nyumbani kati ya nne ilizocheza.

## *Rungu yaibamiza Tuamoyo Daraja la Tatu Kigamboni*

Na Shufaa Lyimo

TIMU ya Rungu FC imeibuka na ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Tuamoyo katika mchezo wa hatua ya sita-bora Ligi Daraja la Tatu Wilaya ya Kigamboni uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Shule ya Msingi Kigamboni, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu Rungu FC, Ahmed Omary, alisema ushindi huo umetokana na wachezaji wake kufuata vema maelekezo aliyowapa katika uwanja wa mazoezi kabla ya mechi hiyo.

Alisema ushindi huo unawapa morali wa kujipanga vizuri kwa ajili ya michezo mitatu ijayo ili kuweza kuendelea kupata matokeo mazuri.

"Wapinzani wetu si wabovu, isipokuwa waliingia katika mfumo na wameadhibiwa, huu ni mwendelezo kuhakikisha michezo ijayo tunapata matokeo," alisema Omary.

Kwa upande wa Katibu wa Mashindano wa Chama cha Soka Wilaya ya Kigamboni (KDFA), Issa Yahya, alisema ushindani ni mkubwa katika ligi hiyo na kwamba kila timu inapambana ili iweze kusonga mbele.

Alisema lengo la ligi hiyo ni kupata timu tano zitakazofuzu kuiwakilisha Kigamboni kucheza Ligi ya Kanda Mkoa wa Dar es Salaam, wakimenyana na Wilaya za Ilala, Temeke, Ubungo na Kinondoni.

## Netiboli Bandari Dar yajipanga Ligi Daraja la Pili

**Na Christina Haule,** Morogoro

MABINGWA watetezi wa mchezo wa netiboli wa mashindano ya Bandari 2023, Timu ya Bandari ya Dar es Salaam, wamesema wanatumia mashindano ya mwaka huu kama sehemu ya maandalizi yao kuelekea michuano ya Netiboli Ligi Daraja la Pili itakayofanyika kuanzia Oktoba 28, mwaka huu mkoani Katavi.

Kauli hiyo ilitolewa jana mkoani Morogoro na Meneja wa timu hiyo, Fatuma Mwinjaka, ambapo alisema pamoja na ukweli kwamba wamefanya maandalizi ya kutosha, ushiriki wao katika mashindano hayo bandari ni sehemu ya kuimarisha kikosi chao kuelekea michuano ya Ligi Daraja la Pili Taifa.

Kwa upande wa Kocha wa timu hiyo, Judith Ilunda, alisema moja ya matarajio yao ni kuwa mabingwa wa mashindano ya Ligi Daraja la Pili.

Timu hiyo ya Bandari Dar es Salaam, ilikubali kipigo cha mabao 34 kwa 31 dhidi ya timu ya Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) huku timu ya TPA Makao Makuu ikiibuka na ushindi wa mabao 35 kwa 20 mbele ya Bandari Mtwara jana.

## ZISIKUPITE

### ALVAREZ KUBAKI CITY

KLABU ya Manchester City ina imani fowadi wa Argentina, mwenye umri wa miaka 23, Julian Alvarez, atasalia katika klabu hiyo licha ya kuripotiwa kuvutia nia ya Barcelona na Real Madrid. ***(Football Insider)***

### LUIZ AWANIWA

ARSENAL bado ina nia ya kujaribu kumsajili kiungo wa kati wa Brazil, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 25, kutoka Aston Villa baada ya ofa kadhaa kukataliwa. ***(90 min)***

### LEWIN AZUA HOFU EVERTON

KLABU ya Everton ina wasiwasi na taarifa ya Al-Ettifaq kutaka kumnunua mshambuliaji wa England, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 26, huku hali ya sintofahamu ya kumchukua ikiendelea. ***(Football Insider)***

### SANCHO BASI TENA

KLABU ya Manchester United iko tayari kwa ofa yoyote ya Januari kwa ajili ya kumuuza Jadon Sancho mwenye umri wa 23, huku kazi ya winga huyo wa kimataifa wa England katika Klabu ya United ikiwa imekwisha kwa asilimia 90. ***(Fabrizio Romano)***

### GONZALEZ AVUTIA EPL

WINGA wa Fiorentina na Argentina, Nicolas Gonzalez mwenye umri wa miaka 25, anavutia klabu kadhaa za Ligi Kuu England baada ya kuanza vema kwa kampeni ya sasa. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### PAVLODIS NA WEST HAM

KLABU ya West Ham inamfuatilia mshambuliaji wa AZ Alkmaar na Ugiriki, Vangelis Pavlidis mwenye umri wa miaka 24, huku wakitafuta kuimarisha safu yao ya ushambuliaji. ***(90 min)***

### PHILLIPS KUHAMA CITY

KLABU ya Manchester City iko tayari na kufikiria kuhama kwa kiungo wao wa kati wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 27. ***(Fabrizio Romano)***

### MURIC AWANIWA SEVILLA

GOLIKIPA wa Burnley na Kosovo, Arijanet Muric mwenye umri wa miaka 24, anavutia klabu kadhaa ikiwamo Union Berlin na Sevilla. ***(Sky Sport)***

### MEJBRI KUNG'OLEWA UNITED

SEVILLA pia wanafuatilia mustakabali wa kiungo wa kati wa Manchester United na Tunisia, Hannibal Mejbri mwenye umri wa miaka 20. ***(Offside).***

### CACERES AWINDWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur ni miongoni mwa timu zinazomfuatilia beki wa kati wa Club America na Uruguay, Sebastian Caceres, 24. ***(Football Insider)***

### DJALO AGOMBEWA MILAN

INTER Milan, AC Milan na Juventus zote zinavutiwa na beki wa kati wa Lille, Tiago Djalo mwenye umri wa miaka 23, huku mkataba wa mchezaji huyo wa zamani wa Kimataifa wa Ureno chini ya umri wa miaka 21, ukikamilika msimu wa majira ya joto. ***(La Gazzetta dello Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# PARTEY SASA AFIKIRIA KUONDOKA ARSENAL

**LONDON,** England

**Hakufurahishwa na kutoanza dhidi ya Chelsea, kambi yake inazidi...**

THOMAS Partey amesikitishwa na nafasi yake iliyopunguzwa Arsenal na atafikiria kutaka kuondoka katika klabu hiyo ikiwa mambo hayataimarika kufikia Krismasi, kwa mujibu wa 90min.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amekosa kucheza kwa sababu ya jeraha alilolipata kwenye sare ya mabao 2-2 na Fulham mwishoni mwa Agosti, na ameona nafasi yake kama kiungo imekuwa kwenye hatihati baada ya ujio wa Declan Rice.**

Partey alianza mechi tatu za kwanza za Arsenal kwenye Ligi Kuu kama beki wa kulia kabla ya kuachwa nje, huku Ben White akiingia kwenye safu ya ulinzi ya kati wakati huo Mikel Arteta akipendelea kuwatumia Rice, Martin Odegaard na Kai Havertz.

Alirejea kutoka kwenye jeraha katika ushindi wa kishindo dhidi ya Manchester City kabla ya mapumziko ya kimataifa Oktoba, lakini hakutumika kama mchezaji wa akiba kwenye sare ya mabao 2-2 na Chelsea katika Uwanja wa Stamford Bridge Jumapili.

Jorginho alichaguliwa na Arteta kuanza mchezo pale Chelsea kabla ya nafasi yake kuchukuliwa na Emile Smith Rowe na Havertz na Leandro Trossard wakabadilishana.

Na sasa Partey hakufurahishwa na kutoanza mchezo huo pale London Magharibi, katika mechi ambayo ilikuwa mojawapo ya mechi kubwa zaidi za Arsenal msimu huu hadi sasa, na kwamba kambi yake inazidi kuchochewa na kupunguzwa kwake kwa dakika.

Kwa hali ilivyo, Partey yuko tayari kurudisha nafasi yake katika upande wa kiungo mkabaji, lakini vyanzo vimethibitisha kwa 90min kwamba atazingatia chaguzi zake wakati wa Krismasi ikiwa hali haijabadilika.

Arsenal walikuwa wameonesha nia ya kumuuza Partey mapema katika dirisha la usajili la majira ya joto, lakini hatimaye waliamua kubaki na Mghana huyo licha ya klabu za Saudia na Juventus kumtaka.

90min ilifichua Jumatatu kwamba 'Washikabunduki' hao bado wana nia ya kumnunua Douglas Luiz wa Aston Villa, baada ya kutuma ofa tatu ambazo hazikufanikiwa mwaka 2022 kwa Mbrazil huyo ambaye alikuwa katika kiwango cha juu.

Mkurugenzi wa Michezo wa Arsenal, Edu pia amekuwa nchini Brazil hivi majuzi akiangalia walengwa wanaoweza kuwasajili huku Andre Trindade wa Fluminense akiwavutia.

## HABARI MICHEZO




# MODRIC HAONDOKI MADRID

**MADRID,** Hispania

MKURUGENZI wa Real Madrid, Jose Angel Sanchez, amekanusha ripoti kwamba Luka Modric anaweza kuondoka kuelekea Saudi Arabia Januari.

Modric amekiri wazi kutofurahia dakika chache alizocheza msimu huu, akiwa ameanza mechi tatu pekee za LaLiga.

Jumla ya dakika 414 za Modric katika mashindano yote ni chini ya wachezaji wengine 14 na inazidi jumla ya Ferland Mendy, Lucas Vazquez, Andriy Lunin, Brahim Diaz na majeruhi Eder Militao.

Ni kwa sababu hiyo ndipo tetesi za kuondoka kwa Modric Januari zimeibuka na Saudi Arabia imetajwa kuwa huenda ikafikiwa, ingawa Sanchez amekanusha uvumi huo.

"Hakuna mazungumzo rasmi kwa upande wa maafisa wa Ligi ya Saudia kumjumuisha Luka Januari, na hatuna maoni yoyote juu ya kuondoka kwake kwenye timu kwa sasa," Sanchez aliiambia Al-Riyadiyah.

Ripoti kutoka nchini Hispania hivi majuzi zilidai kuwa Kocha wa Madrid, Carlo Ancelotti amewakasirisha wasimamizi wa klabu hiyo kwa kumpanga Modric pamoja na mkongwe mwenzake Toni Kroos kutafuta mshindi dhidi ya Sevilla Jumamosi.

Modric na Kroos waliwahi kuwa safu muhimu ya kiungo ya Santiago Bernabeu, lakini wote wameshuka chini ya Ancelotti, ambaye ameshuhudia Madrid ikiweka akiba ya baadhi ya wachezaji makinda wa kati wa mchezo huo.

Federico Valverde, Aurelien Tchouameni na Eduardo Camavinga wote wameibuka nyota, huku kumnunua Jude Bellingham majira ya joto kukiibua mabadiliko ya kimbinu yaliyowaacha Modric na Kroos wakipigania mustakabali wao.

Modric amekataa kuondoa uwezakano wa kuondoka katika klabu hiyo Januari iwapo ataendelea kutatizika kwa dakika, huku waajiri wa zamani Dinamo Zagreb wakitarajia kuungana naye tena.

# Watkins aitaka Euro 2024

**LONDON,** England

OLLIE Watkins amekiri kuwa lengo lake ni kujumuishwa katika kikosi cha England kitakachoshiriki Euro 2024 baada ya kufunga tena Aston Villa ikishinda mabao 4-1 dhidi ya West Ham.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alitengeneza bao la kwanza la Douglas Luiz na kutikisa nyavu kwa mguu wa kushoto huku kikosi cha Unai Emery kikipanda hadi nafasi ya tano kwenye Ligi ya England.


Baada ya kufikisha jumla ya mabao nane katika michuano yote msimu huu, Watkins amepania kung'ara akiwa na 'Simba Watatu' kwenye michuano itakayofanyika chini Ujerumani.

Alisema: "Zaidi ya mabao 20 na kwenda kwenye michuano ya Euro ndicho ninachotaka kufanya. Hayo ndiyo malengo yangu na ndicho ninachokipigania.

"Najua kiwango cha klabu yangu lazima kiwe kizuri nikiwa na Villa."

Juu ya kiwango chake tangu Emery kuwasili, Watkins aliongeza: "Kabla nilikuwa nakimbia kwenye bendera za pembeni na kukimbizana na mambo, lakini sasa tuna mabeki wa pembeni wanaofanya hivyo hivyo, najaribu kukaa kati. Ninafanya mbio za ujanja zaidi, naweza kusema.

"Kuna wakati nilikuwa nikishuka sana ili kupata kugusa mpira wakati sasa sijasumbuka na hilo."






# Akerwa na Spurs licha ya ushindi

**LONDON,** England

ANGE Postecoglou alikasirishwa na kiwango cha Tottenham Hotspur licha ya kuwalaza Fulham kwa mabao 2-0 na kuwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England, Jumatatu.

Heung-Min Son na James Maddison walifunga mabao hayo na kuwapeleka Spurs pointi mbili mbele ya Manchester City na Arsenal, kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

Lakini Postecoglou hakufurahishwa na uchezaji wa timu yake kwa ujumla.

Aliiambia Sky Sports: "Yalikuwa matokeo mazuri. Fulham ni timu ngumu, lakini tuliisimamia vema katika kipindi cha kwanza.

"Nadhani kwa nafasi tulizopata labda tungepata bao la pili na la tatu.

"Kipindi cha pili hakikuwa kizuri kwetu, hatukucheza popote karibu na viwango tulivyoweza, ulikuwa wakati wetu mbaya zaidi wa kumiliki mpira kwa msimu huu.

"Bila mpira bado tulikuwa bora. Bado tuna kazi kubwa ya kufanya.

"Siku zote unatakiwa kuheshimu mchezo. Nimekuwapo kwa muda mrefu vya kutosha kujua kama umejizuia kidogo, inaweza kukuangusha haraka sana.

"Hatukukaa sawa kwa mtindo wa soka, tunaotaka kucheza na tulichukua uhuru na mchezo ambao sikufurahishwa nao."

Ushindi huo umemhakikishia Postecoglou kuvunja rekodi ya kushinda pointi 23 kama kocha mpya ndani ya Spurs baada ya michezo tisa. Lakini Muaustralia huyo alikuwa na nia ya kutozingatia hatua hiyo binafsi.

Aliongeza: "Sichukulii hesabu, si baada ya kipindi cha pili. Kuna kazi nyingi ya kufanya.

# Simba yatolewa AFL kikanuni

INATOKA UKURASA 24

ribia kuwapa wenyeji bao la utangulizi, hata hivyo shuti la Kahraba lilitoka nje kidogo ya lango la Simba.

Dakika moja baadaye Al Ahly walirudi tena kwenye lango la Simba, lakini shuti ya Mohamed Magdy lilipaa juu ya lango huku akiwa kwenye eneo zuri la kufunga.

Simba walijibu mapigo katika dakika ya 11 ambapo shuti la kushtukiza la Mohamed Hussein 'Tshabalala', lilidakwa na golikipa wa Al Ahly, Mohamed El- Shenawy.

Safu ya ulinzi ya Simba iliyokuwa chini ya Malone na Henock Inonga ilifanya makosa mengi kipindi cha kwanza na kama washambuliaji wa Al Ahly wangekuwa makini wangeweza kupata mabao ya mapema.

Simba ilifanya mashambulizi mawili katika dakika ya 19 na 26, lakini umakini mdogo wa winga wake, Denis Kibu uliikosa mabao ya kuongoza.

Dakika ya 24, Kahraba alifanikiwa kufunga bao, lakini hata hivyo lilikataliwa kwa kuwa mfungaji alikuwa ameotea. Mpaka timu hizo zinaenda mapumziko hazikuwa zimefungana.

Kipindi cha pili Simba kwa nyakati tofauti walifanya mabadiliko kwa kuwatoa Kibu, Ntibazonkiza Kanoute na Chama na nafasi zao kuchukuliwa Willy Essomba Onana, Luis Miquissone na Moses Phiri.

Mabadiliko hayo kwa namna nyingine yaliiongezea uhai Simba ambao waliendelea kushambulia na kujilinda huku nyakati nyinginme wachezaji wengi wa Al Ahly wakirudi nyuma kujilinda.

Matokeo hayo sasa yanaifanya Al Ahly kusonga mbele hatua ya nusu fainali na itacheza na mshindi wa jumla kati ya Mamelodi Sundowns na Petro Atletico de Luanda ambao jana usiku walikuwa wanacheza mchezo wa marudiano.

Mchezo wa kwanza uliochezwa Angola, Mamelodi Sundowns waliibuka na ushindi wa mabao 2-0.

# AZIZ KI KINARA MABAO YA FAULO LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Stephane Aziz Ki kufunga mabao matatu 'hat-trick' katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, akiipa timu yake ya Yanga ushindi wa 3-2, idadi hiyo si tu inamfanya kuwa kinara wa ufungaji kwa sasa, bali ameweka rekodi nyingine mpya.

Katika hat-trick hiyo, bao moja la Aziz Ki, lilitokana na mpira wa kutenga (faulo), hivyo linamfanya kuweka rekodi nyingine ya kuongoza kwa kufunga mabao mengi ya faulo mpaka sasa.

Akizungumza juzi baada ya mechi hiyo, mchezaji huyo raia wa Burkina Faso alisema 'hat-trick' yake anaitoa zawadi kwa wachezaji wenzake kwa sababu ndiyo waliofanikisha kufanya hivyo, huku akisema siku zote mchezaji mkubwa lazima uonyeshe kitu tofauti katika mechi kubwa kama hizo.

> **"Nina furaha kufunga 'hat-trick' kwenye dabi hii, ukiwa mchezaji mkubwa ni lazima uoneshe kwamba wewe ni mchezaji mkubwa kwenye mechi kama hizo kuanzia kiwango hadi uwajibikaji.**

Nayatoa mabao haya matatu kama zawadi kwa wachezaji wenzangu kwa sababu walinisaidia kunipa nafasi za kufunga," alisema Aziz Ki.

Mbali na kukaa juu ya kilele cha msimamo wa wafungaji wa Ligi Kuu akiwa na mabao sita na kupiga 'hat-trick' yake ya kwanza msimu huu ikiwa ni ya tatu kwenye ligi, zingine zikifungwa na Jean Baleke wa Simba na Feisal Salum 'Fei Toto' wa Azam FC, Aziz Ki, pia anaongoza kwa kufunga mabao mengi ya faulo mpaka sasa.

Amefunga mabao mawili kwa njia hiyo kati ya mabao tisa yaliyofungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka leo hii kwa faulo.

Juzi alifunga bao kwa mkwaju wa adhabu dakika ya 68 na kuipa Yanga bao la pili, kabla ya kufunga lingine la tatu kwa njia ya kawaida.

Kabla ya bao la juzi, Agosti 29, alifunga bao la faulo kwenye mechi kati ya Yanga dhidi ya JKT Tanzania likiwa ni la kwanza dakika ya 45 na kuiongoza timu yake kushinda mabao 5-0.

Wachezaji wengine waliofunga mabao ya faulo kila mmoja akifunga moja ni Marouf Tshakei wa Singida Big Stars, Edwin Balua wa Prisons, Tariq Seif wa Geita Gold, Omari Kindamba wa Mashujaa FC, Cheikh Sidibe wa Azam FC, Ibrahim Ajibu wa Coastal Union na Martini Kigi wa JKT Tanzania.

## KIBA KAZINI...




Msanii wa Bongo Fleva, Ali Kiba, akitumbuiza wakati wa Tamasha la Serengeti Lite Oktobafest, lililofanyika katika Fukwe za Coco Beach jijini Dar es salaam, mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# 'Yanga inacheza kibingwa'

INATOKA UKURASA 24

rahisi, Azam walicheza vizuri na kuna muda waliuchukua mchezo," alisema.

Alisema kwenye mbio za ubingwa ni timu inapopata ushindi dhidi ya timu zinazoonekana kuwa wapinzani wa karibu inajiweka katika mazingira mazuri kuelekea mwishoni mwa ligi.

"Sasa tunajipanga kwa michezo mingine ya mbele yetu, hatutaki kuangalia matokeo ya wengine, tunaangalia namna gani tunafikia malengo yetu," alisema Gamondi.

Naye Kocha Msaidizi wa Azam FC, Bruno Ferry, alisema kilichowaangusha ni kushindwa kudhibiti mchezo baada ya kuongoza kwa mabao 2-1 kutokana na kukosa uzoefu kwa wachezaji wake, lakini ubora walliokuwa nao wachezaji wa wapinzani wao Yanga.

Alisema ulikuwa mchezo mkubwa uliokutanisha timu mbili kubwa na walijitahidi kupambana kwa kuushika katika baadhi ya nyakati, lakini ubora wa Yanga hasa kiungo Aziz Ki ndio uliwaletea shida na kujikuta wanapoteza mchezo.

"Naipongeza Yanga pamoja na Azizi Ki, alikuwa bora na ndiye amesababisha tukapoteza mchezo, lakini ndio mpira tunarudi kujipanga ili kufanya vizuri mchezo unaokuja lengo ni kubeba ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu," alisema Ferry.

# Netiboli Taifa kujiwinda na michuano ya Afrika

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Kombe la Afrika ya mchezo wa netiboli yanatarajiwa kufanyika Novemba 26 hadi Desemba 6, mwaka huu, nchini Botswana, imeelezwa.

Mashindano hayo yatashirikisha timu 16 ambazo ni nchi Wanachama wa Shirikisho la Netiboli Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (Chaneta), Devota Marwa, alisema muda wowote kuanzia sasa Timu ya Taifa ya Tanzania ya Netiboli, itaingia kambini kwa ajili ya kujiandaa na michuano hiyo.

"Tulitarajia timu yetu iingie kambini mwezi uliopita, lakini tulishindwa kutokana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo wetu, tunaamini katika jitihada serikali kuusaidia timu iweze kuingia kambini moja kwa moja na kuanza maandalizi," alisema Marwa.

Aliongeza kuwa, mashindano hayo hufanyika kila mwaka na kuomba Watanzania waiunge mkono timu yao ili ifanye maandalizi ya kutosha.

Alisema wanatarajia ushindani utakuwa mkubwa katika michuano hiyo kwani kila nchi inahitaji ipate ushindi, lakini akaahidi kurudi na kombe la ubingwa nyumbani.

Michezo
Jumatano Oktoba 25, 2023
Nipashe



Partey afikiria kuondoka Arsenal UKURASA 22

HUNIWEZI...



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza (kushoto), akimiliki mpira dhidi ya beki wa kati wa Al Ahly, Ramy Rabia, katika mchezo wa mkondo wa pili robo fainali ya African Football League, iliyopigwa katika Uwanja wa Cairo, Misri jana na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA YAANDIKA REKODI AFL MISRI

**Na Faustine Feliciane**

## Al Ahly yaitoa kikanuni kwa bao la ugenini huku ikionyesha...

LICHA ya kutolewa kwa kanuni ya bao la ugenini, Simba imeonesha kandanda ya hali ya juu kwa kuweza kuithibiti Al Ahly kwao kwa kutoka sare ya bao 1-1, hivyo kuaga katika michuano ya African Football League (AFL) na wenyeji hao kutinga nusu fainali.

**Al Ahly ya Misri, imesonga mbele kutokana na kikanuni kutokana na mchezo wa kwanza katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kutoka sare ya mabao 2-2, hivyo matokeo ya jumla kuwa 3-3.**

Matokeo hayo yanazidi kuifanya Simba kuanza kujenga rekodi nzuri dhidi ya Al Ahly, ambayo miaka ya nyuma ilikuwa ni vigumu kwao kwenda kupata sare katika Uwanja wa Cairo.

Kwa ujumla timu hizo kila moja imekuwa na rekodi nzuri ya kushinda nyumbani kwake na katika mechi za hivi karibuni kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, mwaka 2019 Simba ilikubali kichapo cha mabao 5-0 nchini Misri kabla ya mchezo wa marudiano Uwanja wa Benjamin Mkapa kushinda 1-0.

Mwaka 2021 kwenye michuano hiyo tena hatua ya makundi, Simba ilishinda bao 1-0 Uwanja wa Benjamin Mkapa na Al Ahly mechi ya marudiano nchini Misri nayo ikapata ushindi kama huo kabla ya msimu huu sare kutawala katika viwanja vyote viwili lakini Al Ahly wakafaidika kikanuni.

Mechi ya jana Simba walihitaji ushindi wowote wa sare ya kuanzia mabao 3-3 kuweza kusonga mbele, lakini hali ilikuwa tofauti baada ya kutoka sare ya 1-1.

Simba ilikuwa ya kwanza kupata bao katika dakika ya 68 kupitia kwa Sadio Kanoute aliyeunganisha mpira wa kichwa kutoka kwa Clatous Chama ambaye aliunganisha krosi safi ya Shomari Kapombe.

Hata hivyo, bao hilo lilidumu kwa dakika saba tu kabla ya Al Ahly kusawazisha kupitia kwa Mahmoud Kahraba katika dakika ya 75.

Al Ahly walianza mchezo kwa kasi na dakika mbili tu tangu kuanza mpira, makosa ya beki Che Malone yalika-

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi: Yanga inacheza kibingwa

**Saada Akida na Faustine Feliciane**

BAADA ya kukiongoza kikosi chake kuibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Azam FC juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema ameanza kuona dalili za ubingwa kutokana na kiwango bora kilichooneshwa na timu yake katika mchezo huo.

Yanga kwa sasa ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa baada ya kufikisha pointi 15 sawa na Simba, lakini mabingwa watetezi hao wakiwa mbele kwa mchezo mmoja.



Akizungumza baada ya mchezo huo, Gamondi alisema wachezaji wake walionesha tabia halisi za timu bingwa na wanahitaji ubingwa msimu huu kutokana na kucheza kwa kujitoa na kutafuta pointi tatu licha ya kutanguliwa.

"Nilitarajia ugumu kwenye mchezo huo, wachezaji wangu wameonesha tabia halisi ya kwamba wapo kwenye timu kubwa inayohitaji ubingwa, tulicheza vizuri kipindi cha pili licha ya kutanguliwa bao la penalti, lakini tulipambana na kusawazisha makosa yetu na kuongeza," alisema Gamondi.

Kocha huyo pia alimpongeza mfungaji wa mabao yote matatu Stephen Aziz Ki, akisema ni mchezaji wa daraja la juu mno kwani pamoja na uchovu aliokuwa nao, alicheza kwa kujitoa kuipigania timu yake kitu ambacho kimeonesha ana mapenzi makubwa na timu hiyo.

Aidha, Gamondi alisema ushindi huo ulikuwa muhimu zaidi kwao katika kujiimarisha na kuongeza hamasa kuelekea michezo ijayo ya ligi hiyo.

"Ushindi ulikuwa muhimu sana, nashukuru tumetimiza malengo yetu japo haikuwa kitu

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >